SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Mpangaji** atuhumiwa kuuza nyumba ya mmiliki mil. 140/-

UKURASA 4



**KIKOSI CHA KWANZA CHENYE ASISTI NYINGI EPL**

UKURASA 12

Nipashe
Jumatatu Februari 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580870
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Washtakiwa ugaidi wapewa dhamana

• **Mchungaji** matatani tuhuma usafirishaji binadamu... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**RADI ILIVYOUA WATU SABA, KUJERUHI 14**
WATU saba wamekufa kwa kupigwa na radi katika matukio mawili tofauti yaliyotokea katika Kijiji cha Milundikwa Kata ya Nkandasi wilayani Nkasi...

UKURASA WA 3
**12 WAHOFIWA KUFA AJALI NDEGE YA Z'BAR**
WATU 12 wanahofiwa kufariki baada ya ndege ya Kampuni ya Flyin Zanzibar yenye namba SH-MZA kuanguka baharini katika kisiwa...

UKURASA WA 4
**CHADEMA KUNUSURU MAKADA WALIOFUNGWA**
ZIKIWA zimepita wiki mbili tangu wanachama wanne wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kata ya Majengo, Halmashauri ya...



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Dk. Ahmed Jaylan ambaye ni Kiongozi wa Ujumbe wa Muslim World League nchini Saudi Arabia, alipotembelea maonyesho ya kongamano la elimu ya dini, lililofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Watanzania waelekezwa pa kukimbilia vita Ukraine

UKURASA 3

## Rais Samia ashuhudia utiaji saini mikataba 36 ya tril. 17/-

UKURASA 2

**MICHEZO** **KASEJA, KOCHA WATOA SIRI USHINDI** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akiongea na wanakikundi wa kilimo cha mwani kilichoko Kijiji cha Mlingotini wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, alipotembelea kikundi hicho katika ziara yake ya kikazi ya siku mbili mkoani Pwani, ili kuimarisha uchumi wa buluu. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Washtakiwa 39 wa ugaidi waachiwa kwa dhamana

**Na Richard Makore,**
MWANZA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Mwanza, imewaachia kwa dhamana washtakiwa 39 wa kesi za ugaidi na kutakiwa kuripoti polisi mara mbili kwa mwezi mfululizo kwa miaka mitatu.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), ililiridhia washtakiwa hao kuachiwa kwa dhamana baada ya kukidhi vigezo na kutakiwa kuendelea kuripoti polisi.

Kadhalika, Jeshi la Polisi mkoani Mwanza linamshikilia mchungaji Diana Bundala wa kanisa la Zumaridi lililoko jijini Mwanza kwa kosa la kufanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Mwanza, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhani Ng'anzi, alisema mahakama imeagiza washtakiwa hao kuripoti ofisi ya DPP mara mbili kwa mwezi mfululizo kwa miaka mitatu.

Ng'anzi alisema washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na makosa mbalimbali yanayohusiana na ugaidi mkoani humo na kwa sasa wameachiwa kwa dhamana.

Alipoulizwa kama washtakiwa hao wapo wanasiasa, hakuwa tayari kutoa majibu ya moja kwa moja na badala yake akaeleza kwamba sheria haiangalii ukubwa wa nafasi ya mtu alionao.

"Hapa hatuangalii kama ni mwanasiasa, sheikh ama mtu kwa nafasi aliyonayo bali tunaangalia suala la sheria za nchi zinasemaje," alisema.

Akizungumzia sakata la mchungaji kufanya biashara haramu, Kamanda Ng'anzi alisema, mtuhumiwa alikamatwa nyumbani kwake akiwa na idadi ya watu 149 wanaoishi kwake. Mchungaji huyo mwenye umri wa miaka 39, mkazi wa Mtaa wa Buguku Buhongwa, anatuhumiwa kuhusika na usafirishaji haramu wa binadamu wapatao 149.

Alisema chanzo cha kukamatwa na kubainika biashara hiyo haramu ni kutokana na mwanamke mmoja kwenda kujificha kwa mchungaji huyo akijaribu kumficha mtoto asiende shule.

Awali Mahakama ya Mwanzo ya Mkuyuni jijini Mwanza ilitoa amri kwa Jeshi la Polisi kumkamata mzazi wa kike wa mtoto, Samir Ally Abbas, ayetakiwa kufikishwa mbele ya mahakama hiyo baada ya kesi ya msingi kusikilizwa.

Kutokana na ukatili huo, mahakama iliagiza Jeshi la Polisi kwenda kumsaka mwanamke huyo pamoja na mtoto wake ambaye ni mwanafunzi.

"Siku ya kwanza askari wetu walienda nyumbani kwa mchungaji huyo, lakini kwa kuwa walikuwa wachache walishindwa kuwakamata mchungaji na watuhumiwa wengine, hivyo askari wetu wakarudi na siku ya pili waliongeza nguvu na kufaninikiwa kuwakamata watuhumiwa hao," alisema Kamanda Ng'anzi.

Alisema baada ya askari kuingia nyumbani kwa mchungaji huyo, walikuta idadi kubwa ya watu na walipofanya uchunguzi walibaini mtuhumiwa huyo alikuwa akifanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu.

Aliongeza kuwa watu hao wametolewa mikoa mbalimbali kisha mchungaji huyo kuwafungia nyumbani kwake kwa lengo la kuwatumikisha na kati yao wanaume 57, wanawake 92.

Katika idadi hiyo wapo watoto 24, wanaokadiriwa kuwa na miaka kati ya 4 hadi 17, ambao wamekatizwa masomo kinyume cha sheria.

Kamanda aliongeza kuwa mchungaji huyo alikuwa akiwaaminisha watu hao kwamba yeye ni Mungu anayeponya, kufufua wafu na kutatua matatizo yao.

Ng'anzi alisema serikali iliwahi kufuta kibali cha kuanzishwa kanisa hilo na kwamba mchungaji huyo alikuwa akifanya kazi za uchungaji bila kibali.

# Samia ashuhudia utiaji saini mikataba 36

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alishuhudia utiaji saini mikataba 36 yenye thamani ya Sh. trilioni 17.35 uliofanyika nchini Dubai katika Maonyesho ya Dubai ya 2020 (Dubai Expo 2020).

Akizungumza baada ya utiaji saini huo Rais alisema kuwa mikataba hiyo ni matokeo ya ushiriki wa Tanzania katika maonyesho hayo, ambapo kwa mara ya kwanza nchi hiyo imepata banda lake peke yake na kutoa fursa kwa zaidi ya Watanzania 400 kuonyesha biashara zao.

Aliongeza kuwa hatua hiyo imechochea kuwapo kwa mfululizo wa mikutano kutoka kwa kampuni zenye nia ya kuwekeza na kufanya biashara katika nchi hiyo kwani wageni wengi waliotembelea banda hilo walivutiwa kukutana na wawekezaji wa Tanzania zaidi kwa ajili ya kujadiliana nao na kufanya makubaliano.

"Na wale waliokwisha kukubaliana wanatamani kujiunga na jamii ya wafanyabiashara wa Tanzania, niwahakikishie kuwa serikali yangu inaendelea kuwatengeneza mazingira bora ya kufanya biashara," alisema Rais Samia. "Ninaamini kongamano la leo litaibua mawazo mapya na yenye tija ya jinsi ya kuimarisha utaratibu wa biashara na uhusiano kati ya washirika walioko humu," alisema.

Naye Dk. Ashatu Kijaji, Waziri wa Uwekezaji, Biashara na Viwanda, alisema mpaka kufikia juzi saa kumi jioni, banda hilo lilitembelewa na watu 17,3417, huku kwa jana peke yake watu 8,408 walitembelea.

Alisema wizara yake pamoja na nyingine zitafanya kazi kwa ukaribu na wawekezaji ili kudumisha uhusiano kwa mustakabali mzuri wa biashara na uwekezaji nchini. Tanzania.

"Tunawakaribisha sana mje tuwekeza pamoja, ninaamini kuwa biashara zinachanua paliko na misingi ya mazungumzo, uaminifu na ushirikiano wa muda mrefu. Mheshimiwa Rais nikuhakikishie kuwa wizara yangu itafuatilia kwa ukaribu kuhakikisha kuwa makubaliano yaliyofanywa hapa yatanufaisha pande zote mbili, " alisema.

Alisema tangu kuanza kwa maonyesho hayo mwaka huu wamefanikia kuratibu programu sita katika kanda mbili zikiwamo za mafuta na gesi, nishati, kilimo na madini. Wamefanikiwa pia kufanya mikutano 126 ya kiserikali na kibiashara wakishirikiana na TANTRADE na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Akiitambulisha mikataba hiyo Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kahyarara, alisema, mikataba iliyosainiwa ipo katika sekta za nishati, habari, viwanda na biashara, kilimo na utalii.

# Radi ilivyoua 7, kujeruhi 14

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WATU saba wamekufa kwa kupigwa na radi katika matukio mawili tofauti yaliyotokea katika Kijiji cha Milundikwa Kata ya Nkandasi wilayani Nkasi na Kijiji cha Luwa Kata ya Ntendo Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa.

Vifo hivyo vimetokana na mvua kubwa zilizonyesha maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Rukwa zikiambatana na radi,

Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, William Mwampaghale, alisema kuwa katika tukio la kwanza lililotokea Februari 26 saa 9 mchana kijiji cha Nkandasi wilayani Nkasi, watu watano waliokuwa wakifanya kibarua cha kupanda maharage shambani walikufa papo hapo, huku 14 kati yao walijeruhiwa baada ya kupigwa na radi wakiwa wamejikinga kwenye kijumba kidogo shambani humo.

Alisema watu hao wakiwa wanaendelea na shughuli zao, baada ya kuona mvua imeanza kunyesha waliacha kupanda maharage na kuamua kukimbilia kwenye kijumba kidogo kilichoko shambani hapo kwa ajili ya kujikinga na mvua.

Kamanda huyo alisema wakiwa wamekaa humo ghafla radi ilipiga kijumba hicho na kusababisha vifo hivyo na kujeruhi wengine.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nkandasi, Given Kisantola, alisema kuwa waliokufa ni wanaume watatu na wanawake wawili, na kwamba majeruhi walikimbizwa katika zahanati ya Jeshi Milundikwa kwa ajili ya matibabu na wengi wao wanaendelea vizuri, huku wengine wakiruhusiwa kurudi nyumbani.

Aliwataja waliokufa ni Yusuph Mbalamwezi (24), Leonard Wayomba (21), Flansisco Kangama, Fazil Mayomba (24), Shukuru Mutayagwa (28) na mtoto Abinet Kazumba (8). Majeruhi ni Veronica Saanane (27), Fobi Mbonile (28), Solostina Sokoni (39), Edina Noel (39), Getruda Mwananjela (34), mtoto Tatu Miyula (10), Teddy Wazamani (37), Mary Kauzeni (18), Daniel Kamilembe (19), Lenatha Chakula (51), Magreth Savery (40), Retisiya Fataki (38) na Velonica Swaila (27).

Kamanda Mwampaghale alisema katika tukio la pili lililotokea siku hiyo hiyo, mwanaume mmoja ambaye jina lake halijajulikana, mkazi wa Kijiji cha Luwa Kata ya Ndendo Manispaa ya Sumbawanga alikufa papo hapo pamoja na mtoto wake baada ya kupigwa radi wakiwa shambani wanalima.

Kutokana na hali hiyo, Jeshi la Polisi limetoa wito kwa wananchi wanapokuwa wanafanya shughuli mbalimbali kuchukua tahadhari kwa kuziacha wanapoona kuna dalili za mvua kunyesha kwani nyakati hizi za masika ni hatari kutokana na kuwapo kwa radi.

HABARI KITAIFA

# Watu 12 wahofiwa kufariki ndege ya Zanzibar ikianguka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATU 12 wanahofiwa kufariki baada ya ndege ya Kampuni ya Flyin Zanzibar yenye namba SH-MZA kuanguka baharini katika kisiwa cha Comoro, ikiwa na marubani wawili.

Akizungumza na Nipashe, Balozi wa Tanzania nchini Comoro, Pereira Ame Silima, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kusema juhudi za kuwatafuta abiria wa ndege hiyo pamoja na marubani wake zinaendelea.

Ndege hiyo iliyoanguka juzi majira ya saa 6:30 mchana ilikuwa na abiria 12 na marubani wawili ambao ni Wazanzibari akiwamo mtoto wa Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Arafat Abdallah Sadala na Mjukuu wa Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Nassor Ahmed Mazuri, ambaye ni Muhammed Mzrui.

Ndege hiyo ilipata ajali wakati ikikaribia kutua katika Uwanja wa Ndege wa Moroni ikitokea katika kisiwa cha Moheli nchini Comoro.

Balozi Pereira alifafanua kuwa vikosi vya uokozi vinaendelea na shughuli za kuwatafuta abiria waliokuwamo katika ndege hiyo, huku baadhi ya mabaki yakielea baharini.

"Bado taarifa haijabadilika...ndege haijaonekana wala abiria, niko katika kikao baadaye tuwasiliane zaidi au nitawajulisha,"alisema Balozi Pereira.

Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano, Usafirishaji na Uchukuzi Zanzibar, Amour Hamil Bakari, alisema wamepokea taarifa za tukio hilo, kwamba wamekuwa wakifuatilia kwa karibu kujua taarifa kamili kupitia ubalozi wa Tanzania ulioko Comoro.

"Ndege imesajiliwa Zanzibar lakini imekuwa ikifanya kazi zake za kutoa huduma za usafiri wa abiria katika visiwa vya Comoro baada ya kukodiwa," alisema.

Msaidizi wa Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Sabri Abdallah, alisema wamepokea taarifa hizo kwa mshtuko mkubwa, kwamba ndugu na familia wanafuatilia kwa karibu taarifa kuhusu tukio hilo.

Sabri alisema msafara wa ndugu na familia ukiongozwa na Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Abdalla Juma Sadalla, umeondoka kuelekea Comoro kwa ajili ya kufuatilia kwa karibu tukio hilo.

Naye Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hadi sasa kijana wao ambaye ni rubani wa pili aliyefahamika kwa jina la Edi Mazrui hajulikani aliko baada ya ndege yao kupata ajali.

Mmiliki wa ndege hiyo, Mazrui Muhammed, alisema kuwa ndege hiyo ilipoteza mawasiliano saa 6:30 baada ya hali ya hewa kubadilika na ndege kupoteza mwelekeo.

# Watanzania walioko Ukraine waelekezwa mahali pa kukimbilia

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imewataka Watanzania walioko nchini Ukraine kutafuta hifadhi katika nchi za Poland na Romania ambako kuna utulivu.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali katika wizara hiyo, Emmanuel Buhohela, ilieleza kuwa serikali inaendelea kuchukua hatua za haraka kwa Watanzania wanaoishi nchini humo.

"Kutokana na hali ya usalama kuendelea kuzorota nchini Ukraine, serikali inaendelea kuchukua hatua za haraka ili Watanzania takribani 300 walioko nchini humo kuondoka na kuingia katika nchi za Poland na Romania ambako kuna utulivu. Hatua hii itatoa fursa kuwawezesha raia wetu kurejea nchini kwa usalama," ilieleza taarifa hiyo.

Pia ilieleza kuwa mpaka sasa hakuna Mtanzania yeyote aliyepata madhara kutokana na hali inayoendelea nchini Ukraine.

Kadhalika, imewaomba wazazi wa wanafunzi, ndugu na jamaa wenye wapendwa wao nchini Ukraine, kuendelea kuwa watulivu katika kipindi hiki ambacho serikali inaendelea kuchukua hatua hizo.

HABARI ZAIDI UK. 19

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO**

Mimi ABASI ATHUMANI wa Simu Na.0655 162416 TANGA, mtu mzima na akili zangu timamu mkazi wa Mtaa wa Makorora Tanga, bila ya kushawishiwa na mtu yeyote naapa kama ifuatavyo:-

- KWAMBA, mimi ABASI ATHUMANI ndiye mmiliki halali wa kiwanja Na. 514 kitalu "B" kilichopo New Nguvumali katika Halmashauri ya Jiji la Tanga.
- KWAMBA, hati ya umiliki wa kiwanja hicho imepotea na hakuna tena uwezekano wa kupatikana. TAARIFA POLISI: DAR/MAG/RB/79126/2022.
- KWAMBA, kwa kiapo hiki naiomba Idara ya Ardhi inipatie Hati ya nyumba hiyo.

**UTHIBITISHO**
**Mimi ABASI ATHUMANI,** nathibitisha kuwa yote niliyoyasema hapo juu kuanzia aya ya 1-3 ni kweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sheria ya viapo (The Oaths and Statutory Declaration Act.Cap.34 R.E 2002)

**MBELE YA.....H.A MAJANI**
**CHEO...HAKIMU MKAZI**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**MATRIMONIAL CIVIL CASE 2/2021**
**JALIWA HOSIANA MAHENGE ……………. PLAINTIFF**
**V/S**
**DEBORA GEORGE NDAHANI……………DEFENDANT**

**TO DEBORA GEORGE NDAHANI**

Whereas your attendance is required to ……………………on behalf of the…………………in the above suit you are hereby required personally to appear before this court on the 02 day of 03……2022 at 9.00 O'clock in the forenoon.
If you fail to comply with this order without lawful excuse you will be subject to the consequence of the attendance laid down in rule 12 of order XVI of the code of civil procedure 1966 CAP 33 R.E 2002.

**Given under my hand and the seal of the court this 23 day of 02,2022.**

COURT SEAL DODOMA DISTRICT

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

Ndugu RENATHA SOSTHENES MUHIZA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA IST yenye namba za usajili T 513 DMK. Yenye Chassis No: NCP650031615 Na. Engine No: 1NZB395208 Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: TAN/RB/81866/2022





Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Ali (katikati), akimkabidhi msaada wa vyakula na mafuta ya kupikia, mkazi wa Mkuranga mkoani Pwani, Atibu Nasibu (kushoto), vilivyotolewa na Taasisi ya Afrika Relief Organizational kwa kushirikiana na Taasisi ya Rahma International Society za nchini Kuwait katika kuadhimisha Siku ya Uhuru wa taifa hilo, kwa ajili ya kuwasaidia baadhi ya wakazi wa wilaya hiyo juzi. Wapili kushoto ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Rahma International Society, Abdul Aziz Alinzy na (wapili kulia) ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Afrika Relief Organizational, Samy Mohamed, na Sheikh Othuman Kapolo (kulia). **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mpangaji adaiwa kuuza nyumba aliyopangishwa

**Na Richard Makore,** GEITA

MPANGAJI katika nyumba namba 20 Kitalu 'A' iliyoko barabara ya Uhuru Geita Mjini, Kudra Rajabu, anadaiwa kuuza nyumba aliyopangishwa na mmiliki wake, Kwitega Maganga.Kudra anadaiwa kuuza nyumba hiyo aliyokuwa akiishi na mume wake kwa gharama ya Sh. milioni 140, pasipo mmiliki wake kufahamu.

Mmiliki wa nyumba hiyo, alibaini nyumba yake kuuzwa baada ya kuona kundi la vijana likibomoa, alipofika eneo hilo kuulizia kinachoendelea alikamatwa na wahusika na kumpiga kisha kufungwa.

Akizungumza na Nipashe Mjini Geita, mmiliki wa nyumba hiyo (Maganga) alisema, aliwapangisha wanandoa hao miaka mingi iliyopita na hakuwahi kuwa na wasiwasi nao kwa kuwa na yeye anaishi eneo hilo la Geita Mjini.

Alisema alinunua kiwanja hicho na kupewa hati mwaka 1987 na kwamba alijenga nyumba na kuwapangisha watu hao.

Maganga alisema anachofahamu ni kwamba mpangaji wake (Kudra), aliwahi kumkopesha Sh. 900,000 bila maandishi yoyote na alizilipa.

Maganga alisema ashangaa kuona mpangaji wake akaingia tamaa na kuuza nyumba yake kwa Sh. milioni 140, bila yeye kujua.

Akisimuliza zaidi, Maganga (mmiliki wa nyumba) alisema baada ya mpangaji huyo kumkopesha fedha hizo alimwomba ampe na hati kama dhamana na kwamba alimpatia.

Alisema baada ya kumaliza mkopo huo alienda kuomba hati yake ndipo Kudra (mpangaji) alipomwambia imepotea na hivyo kuamua kwenda polisi kutoa taarifa.

Maganga alisema licha ya kutoa taarifa polisi, lakini alitoa taarifa kwa Kamishna wa Ardhi mkoani Geita na kuomba waangalie endapo hati yake kwa sasa inatumiwa na mtu mwingine. Alisema baada ya maofisa ardhi kuangalia walimwambia kwamba bado hati hiyo inasomeka kwa jina lake.

Nipashe lilimtafuta mpangaji huyo, alikana tuhuma hizo na kusema kwamba Maganga (mmiliki wa nyumba) alimuuzia nyumba hiyo bila maandishi mwaka 1999.

Hata hivyo, Kudra alikiri kuuza nyumba hiyo na mume wake baada ya mahakama kutoa talaka, hivyo hiyo ilikuwa ni sehemu ya mali walizokuwa nazo.

Alisema waliuza kwa gharama ya Sh. milioni 140 na kwamba ni mali yao halali kwa kuwa waliinunua kutoka kwa Maganga ingawa hawakuandikishana popote.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyerere, Dua Issa Kaburi, alikiri kufahamu mgogoro huo.

Alisema taarifa alizonazo ofisini kwake ni kwamba Kudra alinunua nyumba hiyo ingawa hapakuwa na maandishi yoyote wala shahidi, jambo ambalo linampa nguvu Maganga ambaye anamiliki hati ya kiwanja hicho.

Kaburi alisema kutokana na hatua hiyo, mtu aliyenunua nyumba hiyo naye hana hati ya kumiliki kiwanja hicho kisheria.

Maganga aliiomba serikali kuingilia kati mgogoro huo ili kumsaidia kupata nyumba yake.

# CHADEMA kuwakatia rufani makada waliofungwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

ZIKIWA zimepita wiki mbili tangu wanachama wanne wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kata ya Majengo, Halmashauri ya Mtama, Wilaya na Mkoa wa Lindi wahukumiwe kifungo cha miaka minane gerezani, uongozi wa chama hicho umeanza mchakato wa kukata rufani kujaribu kuwaokoa.

Mwenyekiti wa chama hicho Wilaya ya Lindi, Idd Mandindi, aliyasema hayo katika mahojiano na Nipashe, lililotaka kufahamu hatua zinazochukuliwa katika kujaribu kuwanusuru wanachama wao waliofungwa gerezani kwa makosa ya kuharibu mali na kujeruhi watu iliyotolewa na Mahakama ya Mkoa wa Lindi.

Wanachama waliohukumiwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Lindi baada ya kupatikana na hatia ya kuharibu mali wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2020, ni Rajabu Hassani, Hamisi Maleje, Moshi Hamisi na Dadi Shayo, wote wakazi wa Kata ya Majengo, Halmashauri ya Mtama.

Mandindi alisema wameshaanza mchakato kwa kutoa taarifa ya kusudio hilo kwa uongozi wenzao wa kanda na hadi Taifa.

Mandindi alisema licha ya kutoa taarifa ngazi ya Taifa, pia wanaendelea na taratibu za kwenda Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi Mkoa wa Lindi, kufuatilia nakala ya hukumu na mwenendo wa kesi husika.

"Mchakato tayari umeanza kuwaokoa wanachama wetu waliofungwa na sasa tumefika hapa mahakamani kufuata nakala ya hukumu na mwenendo wa kesi,"alisema Mandindi.

Alipoulizwa kama wapo tayari kushirikiana na wenzao wa Chama cha ACT-Wazalendo, walionyesha nia ya kukata rufani ili kuwaokoa wanachama hao, Mandindi alisema kwamba hawapo tayari kushirikiana na chama chochote cha siasa.

Mwenyekiti huyo alisema wapo katika maandalizi ya kuwasilisha rufani yao Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara, muda wowote baada ya kukamilisha taratibu zinazohitajika kwa mujibu wa sheria.

Februari 19, mwaka huu, wakati wa mkutano wa ACT-Wazalendo uliofanyika Mjini Lindi, mwenyekiti wake ngazi ya mkoa, Rashidi Mchinjita kwa niaba ya chama chake alitangaza nia ya kukata rufani kupinga hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Lindi dhidi ya wanachama wa CHADEMA.

# Ndalichako atoa neno kwa PSSSF, Magereza kiwanda bidhaa za ngozi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amepongeza uwekezaji kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) pamoja na Jeshi la Magereza kwa hatua nzuri ya ukamilishaji wa kiwanda cha uzalishaji bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro (Kilimanjaro International Leather Industries Co. Ltd).

Waziri Ndalichako alitoa pongezi hizo juzi baada ya kupokea taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro wakati alipotembelea kiwanda hicho kwa lengo la kukagua maendeleo ya kiwanda na kuangalia namna ya uzalishaji wa bidhaa.

Alisema kuwa, amefurahishwa na uwekezaji katika kiwanda hicho ambacho kitatoa ajira nyingi kwa vijana pamoja na kuchangia ukuaji wa pato la Taifa kupitia bidhaa zitakazokuwa zinazalishwa na kiwanda hicho.

"Kiwanda kimefikia hatua nzuri na mashine zote zimeshafika, hatua inayoendelea ni kuziunganisha mashine hizo ili uzalishaji uendelee kufanyika wanatengeneza. Viatu vinavyotengenezwa hapa ni vizuri na wanatengeneza viatu vyenye mitindo ya aina mbalimbali," alisema Prof. Ndalichako.

Aliongeza kuwa, uwepo wa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro kutachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la ajira nchini baada ya kukamilika kwa kiwanda hicho.

"Kiwanda kinauwezo wa kuajiri watu zaidi ya 10,000 ambapo ajira za moja kwa moja ni 3,000 pamoja na ajira zaidi kwa Watanzania kutokana na fursa mbalimbali zitakazo kuwapo kiwandani hapo," alisema.

Aidha, Waziri Ndalichako aliwasihi watendaji wa kiwanda hicho kuhakikisha malengo ya uzalishaji katika kiwanda yanazingatiwa ili fedha zilizowekezwa zitumike kwa matokeo yaliyokusudiwa.

Kadhalika, aliwapongeza Uongozi wa Chuo cha VETA pamoja na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kwa kutoa mafunzo bora kwa vijana ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi, huku akibainisha kuwa vijana wanaotoka katika vyuo hivyo wamekuwa watengenezaji wazuri wa viatu. Hivyo alitoa wito vijana kuchangamkia sekta ya ngozi kwa kuwa serikali imeanza kuwekeza katika kiwanda cha ngozi na kutakuwa na uhitaji wa rasilimali watu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha bidhaa za Ngozi cha Kilimanjaro, Mhandisi Masud Omary, alieleza kuwa menejimenti ya kiwanda hicho imejipanga kuendelea kukuza masoko ya bidhaa zinazozalishwa kiwandani hapo ili kuhamasisha wananchi kununua bidhaa hizo. Pia alieleza juhudi zinazofanywa na kiwanda katika kukuza soko la bidhaa nje ya nchi.

# Wizi wa mafuta sasa watishia mradi SGR

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA



VITENDO vya wizi wa mafuta ya magari na mitambo mingine katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), vinatishia kurudisha nyuma juhudi za serikali kukamilisha miradi ya kimkakati kwa wakati.

Tuhuma za wizi huo wa mafuta ziliibuliwa na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (pichani), mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kutembelea mradi huo.

Mboneko alisema ikiwa wizi huo utaendelea, atawafukuza kazi madereva wote wanaofanyakazi hapo na kupeleka vijana wengine wenye uzalendo.

Alisema madereva hao wamekuwa na tabia ya kuiba mafuta na kuyahifadhi kwenye makazi ya watu, kitendo ambacho kinahujumu mradi huo.

Mboneko alifanya ziara hiyo ili kuona maendeleo ya ujenzi wa mradi huo pamoja na kuzungumza na wananchi na wafanyakazi katika eneo hilo. Alisema anasikitishwa kuona madereva wanaiba mafuta na kushindwa kuwa wazalendo katika nchi yao badala yake wanaipa hasara serikali.

"Madereva ambao mmepata ajira kwenye mradi huu wa ujenzi wa SGR, kipande hiki cha tano sijapendezwa na tabia yenu mmekithiri sana kwa wizi wa mafuta na hivi karibuni tulikamata madumu 37 ya mafuta yakiwa yamefichwa kwenye makazi ya wananchi, acheni tabia hiyo mara moja huko ni kuhujumu mradi huu," alisema Mboneko.

Aidha, alisema kitendo cha kuficha mafuta kwenye makazi ya wananchi ni hatari utakapotokea moto kuwaka katika makazi yao.

Katika hatua nyingine, Mboneko alisema suala la malalamiko yao juu ya mikataba mibovu atalifanyia kazi na tayari ameshatoa maagizo kwa naibu meneja wa mradi huo kipande hicho cha tano.

Aliwatoa wasiwasi wananchi ambao mradi huo umepita kwenye mashamba yao na makazi kwamba kila mtu atalipwa fidia kwa mujibu wa sheria.

Ofisa operesheni kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Shinyanga, Inspekta Edward Lukuba, alisema kitendo ambacho wanakifanya madereva hao kuhifadhi mafuta kwenye makazi ya watu ni hatari ikitokea ajali ya moto.

Naibu meneja wa mradi huo, Alex Bunzu, alisema maagizo yote yaliyotolewa kwao atayatekeleza likiwamo suala hilo la ulipwaji wa fidia na utoaji wa mikataba kwa wafanyakazi.

Aliwataka vijana wanaofanyakazi katika mradi huo kuwa wazalendo na nchi yao na kuacha tabia ya wizi wa vitu mbalimbali.

Akizungumzia ujenzi wa mradi huo, alisema umefikia asilimia 4.5 na utakamilika mwaka 2024 kwa gharama ya Sh. trilioni 3.

Baadhi ya madereva hao walisema wapo wanaojihusisha na wizi huo wa mafuta kutokana na malipo kuwa kidogo ambayo ni Sh.12,500 kwa siku.

## Viongozi Mtwara waweka malengo 7 kuongeza ufaulu

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

UONGOZI wa Mkoa wa Mtwara umeweka malengo saba ya kufanyia kazi kuhakikisha mkoa huo unafanya vizuri katika sekta ya elimu.

Mojawapo ya lengo ni kuhakikisha wanafunzi kuanzia darasa la kwanza hadi la saba wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Lengo lingine ni kuhakikisha wanaongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi kwa ngazi ya sekondari hadi kufikia asilimia 60 ifikapo mwaka 2025, kutoka asilimia 23 za sasa.

Malengo hayo yaliainishwa na Ofisa Elimu Mkoa wa Mtwara, Kiduma Mageni, akiwa kwenye ziara ya mkuu wa mkoa huo, Brigedia Jenerali, Marco Gaguti, walipotembelea halmashauri zilizo katika Wilaya ya Mtwara na Newala kwa ajili ya kufuatilia mpango kazi wa elimu wa mkoa huo. Mageni alisema mkoa ulifanya uchambuzi yakinifu wa changamoto zinazokabili katika elimu ya msingi ambayo ni kuanzia elimu ya awali mpaka kidato cha nne na kuja na maazimio hayo saba kwa kuyapa kipaumbele.

Alisema kimkoa wamedhamiria kuifuta kabisa changamoto hiyo licha ya kuwapo uhaba na kwamba wataweka juhudi za makusudi kuwajengea msingi wanafunzi.

Alitaja lengo la tatu ni kuhangaika na mdondoko wa wanafunzi kwa kile alichoeleza wapo wanafunzi ambao ni watoro wa reja reja na wengine ni watoro wa kudumu, hali inayofanya wengi walio katika makundi hayo kushindwa kwenda sambamba na wenzao wanaohudhuria darasani bila kukosa. Alisema katika lengo hilo dhamira yao ni kuhakikisha kila mwanafunzi anayeandikishwa darasa la kwanza ajifunze na afundishwe ipasavyo na aende hatua moja baada ya nyingine ikiwa ni pamoja na kufaulu mitihani kati ya darasa la pili la nne la saba kidato cha pili na nne.

Alitaja malengo mengine ni kuimarisha uwajibikaji wa viongozi elimu kuanzia ngazi ya msingi, shule za msingi na sekondari, waratibu elimu kata, maofisa elimu wa halmashauri na halmashauri kwa ujumla wakiwamo wakurugenzi mpaka mkoani ili kuwe na uwajibikaji wa pamoja kufikia malengo hayo.

Alitaja lengo la saba kuwa ni kuimarisha ushiriki na ushirikiano na umiliki wa shughuli za elimu kwa jamii na wazazi kwa kufanya uhamasishaji wa kila mara juu ya kutekeleza wajibu wao.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Gaguti, alisema uwekezaji uliofanywa na serikali katika eneo la elimu kwenye mkoa huo, hauendani na matokeo yanayopatikana, huku akieleza kuwa matokeo yaliyopita asilimia 72 ya wanafunzi walipata daraja sifuri na daraja la nne.

## RC Hapi awaonya wafanyabiashara

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKUU wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi, amewahimiza wafanyabiashara mkoani hapo kufuata taratibu na sheria za ulipaji kodi na ushuru mbalimbali kwa hiari baada ya kupata elimu ya ulipaji kodi kwa kwa kutembelea wafanyabiashara 4,014 kwenye maeneo ya biashara zao, huku akiwaonya wasio waaminifu.

Amesema wafanyabiashara wasio waaminifu wanafanya biashara za magendo katika vijiji vya mipakani na kuikosesha serikali mapato ambayo yangefanya maendeleo na kwamba hatua kali zitachukuliwa kwa wakwepa kodi na wafanya magendo kwani wanahujumu uchumi wa taifa.

Alikuwa akizungumza katika mkutano wa hadhara na wakazi wa Mji wa Sirari mwishoni mwa wiki, huku akiongozana na kamati yake ya ulinzi na usalama ya mkoa na Wilaya ya Tarime.

Aliwapongeza maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kufika mkoani Mara na kuwatembelea wafanyabiashara na kutoa elimu katika maeneo yao ya shughuli zao wafanyabiashara 4,014 kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari na faida zake. Wafanyabiashara aliowaonya kwa kufanya biashara za magendo ni wa vijiji vya mipakani vikiwamo Kubiterere, Kogaja, Nyamohonda, Sirari, Borega, Kegonga kwa kuwa kukwepa kulipa kodi halali ni kosa la jinai kwa kuikosesha serikali mapato kwa ajili ya maendeleo.


Agriwezesha

## JOB VACANCIES

Agriwezesha is a Non-Governmental Organization working closely with small-holder farmers in Tanzania to enhance agricultural productivity by providing training and consultations on modern farming practices as well as improving farmers' market connections and supporting sustainable agriculture. Our head quarter is based at Morogoro Municipal. Agriwezesha is currently looking for qualified candidates to fill in the following positions in multiple locations;

**Agricultural Technicians 6 (Six) Positions**
**Key responsibilities**
- Provide technical advice to smallholder farmers on agroforestry
- Provide technical advice as well as trainings to smallholder farmers on land management, conservation and rehabilitation
- Assist on plant propagation, seedling growth, irrigation regimes, weed maintenance as well as transplanting
- Maintain accurate records including management and coordination of databases for nursery production records
- Create and review standard procedures for nursery tasks to enable efficient on daily operations
- Create and review standard procedures for transplanting tasks to enable efficient on daily operations
- Report all planted trees into the digital system accordingly
- To provide all required reports as per the organization standards

**Required Skills**
- Good project management skills
- Good computer applications skills.
- Good organizational skills.

**Preferred Qualifications**
Diploma/Bachelor in Agriculture General/Horticulture/ Agronomy/ Forestry and other related fields with at least one year working experience in relevant field.
Knowledge in GIS and Remote Sensing will be added advantage

**Monitoring and Evaluation Officer 1 (One) Position**
**Key responsibilities**
- Develop and implement a robust monitoring and evaluation system that will ensure tracking of project/ programme results at different levels (outputs, outcomes and impact)
- Work with other managers to ensure the collection of relevant and appropriate data needed which will be utilized in monitoring strengths, weaknesses and gaps in existing projects and programs and services and for reporting
- Develop M&E plans for all projects and proposals and ensure the same is followed up during implementation;
- Ensure all grants have updated work-plan and performance management plan in tandem with all approved proposals, regularly reviewing and updating as needed
- Assist in the revision of the project log frame matrix, particularly in the areas of performance indicators and their measurement;
- Collect data on a regular basis to measure achievement against the performance indicators

**Required Skills**
- Good knowledge of programme implementation, monitoring and evaluation techniques and practices.
- Familiarity with impact assessment will be added advantage
- Good computer applications skills.
- Good organizational skills.

**Preferred Qualifications**
Diploma/Bachelor in Forestry/ General Agriculture/Horticulture/Agronomy with at least one year working experience in relevant field.
Knowledge in GIS and Remote Sensing will be added advantage

**HOW TO APPLY**
Interested candidates may apply by sending application letters, resumes and photocopies of certificates through **info@agriwezesha.co.tz** for more details visit our website **www.agriwezesha.co.tz .**
**Closing date is 15th March 2022.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, TPLB mkilala waamuzi wataamua bingwa wa ligi

**LIGI** Kuu Tanazania Bara tayari imeingia mzunguko wa pili ambao ni walala salama kabla ya bingwa atakayeiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika kujulikana mwishoni mwa msimu huu wa 2021/22.

Lakini mwishoni mwa mzunguko huu ndio utakaoamua timu mbili zitakazoshuka daraja moja kwa moja kwenda kucheza Ligi ya Championship na zile zitakazoshika nafasi ya 13 na 14 ambazo zitacheza mechi za mtoano 'play off' dhidi ya timu zitakazoshika nafasi ya pili kutoka Kundi A na B kwenye Championship ili kuwania nafasi mbili za kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Kwa ujumla ni mzunguko mgumu kwani si hilo tu, bali raundi hii ya lala salama pia ndiyo ambayo itaamua dau ambalo kila timu italipata kutokana na nafasi itakayomaliza, hii ni kutokana na hadhi iliyoongezewa na wadhamini wa haki za matangazo ya televisheni, Azam Media Limited kwa kuweka bonasi itakayolipwa kwa kila timu kulingana nafasi itakayomaliza mwishoni mwa msimu.

Kwa mujibu wa mkataba ambao Azam Media Limited na Shirikisho la Soka nchini (TFF), wameingia bingwa wa Ligi Kuu atapata bonasi ya Sh. milioni 500, huku mshindi wa pili akiondoka milioni 250, wa watatu milioni 225, wanne Sh. milioni 200, nafasi ya tano milioni 65, ya sita milioni 60, ya saba milioni 55 huku dau hilo likienda likipungua hadi kwa timu itakayoburuza mkia.

Pamoja na hayo yote, huu ni mzunguko ambao kila mchezaji hata kutoka timu zinazoburuza mkia atataka kuonyesha uwezo wake ili kujitafutia soka la kubaki Ligi Kuu ama kujiuza klabu kubwa zaidi ndani na nje ya nchi. Hivyo, tunatarajia kuona waamuzi wakichezesha kwa umakini zaidi kwa kufuata sheria zote 17 bila kuibinya timu yoyote ili mwisho wa msimu kila moja ivune ilichostahili bila kuwapo manung'uniko yoyote.

Tunatambua klabu imewekeza kiasi kikubwa cha fedha na kila moja ina malengo yake kama si kutwaa ubingwa ni kushika nafasi nne za juu ili kujihakikishia bonasi kubwa kutoka kwa wadhamini, lakini pia kuanzia sasa zipo zinazopigana kuepuka kushuka daraja.

Kosa moja ambalo linaloweza kufanywa na mwamuzi kwa kutoa maamuzi ya kutatanisha yatakayoinyima ushindi timu moja dhidi ya nyingine linaweza kuwa kuwa chanzo cha kupoteza ubingwa, kukosa nafasi za juu ama kushuka daraja kabisa.

Hivyo, hatutaki kuona makosa ambayo yametokea mzunguko wa kwanza kutoka kwa waamuzi yakijirudia tena raundi hii ya lala salama jambo ambalo tunawakumbusha waamuzi kuongeza umakini, lakini Bodi ya Ligi (TPLB), TFF na hata Chama cha Waamuzi nchini (FRAT), kuzidi kuwamulika wale wote wanaovurunda na kuwachukulia hatua kali ili wasiwe chanzo cha kutuamulia bingwa na timu za kushuka daraja na zile za kucheza mtoano.

Pamoja na hayo yote lakini FRAT haina budi kuwakalisha kitako waamuzi mara kwa mara na kuwakumbusha wajibu wao katika maamuzi wanayoyatoa hususan ili kuzidi kutenda haki katika ligi hiyo ambayo kwa sasa ni ya 13 kwa ubora Afrika.

Nipashe tunataka kuona malalamiko dhidi ya waamuzi ambayo yalijitokeza mzunguko wa kwanza yakimalizika kabisa ili mwisho wa msimu pasiwe na timu inatoa kisingizio katika nafasi iliyomaliza.

Si hilo tu, bali pia tunatambua bila kuwa na bingwa aliyestahili, tutaishia kupata mwakilishi mbovu kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao, ambaye atakwenda kulitia aibu taifa kwa kutolewa raundi ya awali.

Lakini kama Klabu ya Simba itafanikiwa kufika mbali msimu huu kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, ni wazi itakuwa imetetea nafasi nne za Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano ya CAF msimu ujao, hivyo kama waamuzi hawatatenda haki ni wazi nchi itapeleka wawakilishi wabovu katika nafasi hizo nne jambo ambalo hatutaki kuliona likitokea.

Lengo letu ni kuona timu zote zitakazopata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao zikifika angalau robo fainali na kuendelea, hivyo njia pekee ni kuanzia sasa waamuzi kutoibeba timu yoyote kwenye Ligi Kuu kwa namna yoyote ile.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Mzunguko wa pili timu zisiende na matokeo

**MZUNGUKO** wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara umeanza, huku kila timu ikitarajiwa kucheza mechi 15 zingine ili kumalizika mechi 30 za msimu wa 2021/22.

Jumla ya timu 16 zinashiriki ligi hiyo, na tayari zimeshaanza kujigawa, japo mpaka sasa huwezi kutabiri ipi itakuwa bingwa, zitakazobaki Ligi Kuu na kushuka daraja.

Simba na Yanga zinaonekana ndizo timu ambazo zimejipambanua kuusaka ubingwa kwa udi na vumba. Azam FC, Namungo na Mbeya City zinaonekana ni kama timu zinazonyatia. Zimejiweka kwenye eneo lao ambalo zinaziangalia timu za Simba na Yanga kama zitazubaa kwenye harakati zao za kusaka ubingwa basi moja kati ya timu hizo zinaweza kuupata.

Pia timu hizo zinaonekana kuvizia zile ambazo huwa zinapatikana kama nchi itapeleka timu nne kwenye mechi za kimataifa, basi angalau timu moja au mbili kati ya hizo iwe mojawapo.

Zipo timu ambazo zipo kati, lengo lao kubwa ni kuwa eneo salama. Zinacheza Ligi Kuu kwa kutaka tu zipate pointi tatu ziwe katikati, hazipo juu wala chini, ili mradi tu zinataka msimu ujao ziendelee kula matunda ya Ligi Kuu.

Hata hivyo, kuna timu ambazo hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza ziko hoi bin taaban. Zinaonekana hazijiwezi na huenda kama hali itaendelea kuwa mbaya kwenye mzunguko wa pili, zinaweza kushuka daraja. Timu hizo ni Prisons, Mbeya Kwanza, Ruvu Shooting, Mtibwa Sugar na hata Biashara United. Hata hivyo, hakuna timu yoyote inayopenda kushuka daraja kirahisi.

Hadi mapema jana, msimamo wa Ligi Kuu ulikuwa unaonyesha kuwa kuna tofauti ya pointi 13 tu kati ya timu ya mwisho Prisons yenye pointi 11, na Azam pamoja na Namungo ambazo kila moja ilikuwa na pointi 24, ukiziondoa timu za juu, Simba na Yanga.

Hii inaonyesha kuwa kuna tofauti ndogo kati ya timu zinazoshika kuanzia nafasi ya tatu hadi ya mwisho ambayo ni ya 16. Ina maana lolote linaweza kutokea.

Kwa maana hiyo, mzunguko huu wa pili unaweza kuwa mgumu na wenye msisimko zaidi kuliko ule wa kwanza.

Kwa bahati nzuri au mbaya, tulichokishuhudia kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza ni kwamba timu nyingi za Ligi Kuu zina uwezo unaolingana.

Timu A ina uwezo wa kuifunga timu B bila matatizo yoyote, na huenda zikirudiana, timu ile iliyofungwa ikawa na uwezo wa kuifunga nyingine bila shida yoyote. Hata zile timu zinazoitwa au kujiita kubwa na kongwe, zinazidi timu nyingine kidogo kwenye uzoefu na ukomavu wa wachezaji wao tu, lakini si uwezo wa kitimu kwa ujumla.

Tulichoshuhudia kingine kwenye timu hizi ni mbinu za makocha. Wingi wa makocha, hasa kutoka nje ya nchi umesababisha baadhi ya timu kuacha kutumia vipaji vya mchezaji mmoja mmoja, badala yake kucheza kwa mfumo ambao umekuwa ukiwapa matokeo mazuri wakati mwingine.

Vyote hivi ukijumlisha, utagundua kuwa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kama waamuzi watapunguza makosa yao ya kibinadamu na yale mengine ya nia zao 'ovu', tunaweza kushuhudia vitu tofauti na jinsi ambavyo tunadhani.

Kuna timu zitakataa kuwa ngazi za timu zingine kwenda kutwaa ubingwa. Zipo zitakazoshtuka na kuanza kutoka shimoni, na kutaka kubaki Ligi Kuu.

Kitendo cha timu za chini kushinda, kutazishtua zile za juu yake ambazo nazo zitataka kushinda kwa lazima, hata kama hazitoweza kutwaa ubingwa, sababu tu ikiwa ni kutopitwa kwa pointi na timu za chini, kwani kitendo cha kukaribiwa pointi ni hatari kwao, kwani kibao kinaweza kugeuka.

Natoa rai tu kwa wanachama na mashabiki wa timu mbalimbali kutokwenda na matokeo yao mfukoni kwenye mechi za mzunguko wa pili, kwani ni kipindi ambacho kila mmoja ana malengo yake.

Hakuna timu itakayotaka kudondosha pointi mbili au tatu kirahisi. Mechi zitakuwa ngumu, siyo tena tuanze kusikia maneno kuwa tunaonewa.

Kuna baadhi ya timu utafikiri zenyewe ndizo zilipangiwa kushinda tu kwenye dunia hii na zingine hazina haki hiyo.

Ni wakati wa kujiandaa kisaikolojia, isije tukaanza kusikia eti kuna timu zinapewa pesa ili zikamie, au waamuzi wanawanyima penalti na dakika za nyongeza, na kuzipa timu nyingine. Ligi ni ngumu na kila timu inapambana kushinda. Timu ikishindwa itafute sababu za kiufundi na si vinginevyo.



Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha, Elipid Tesha, akimwonyesha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi), Dk. Ally Possi, eneo la mradi wa ujenzi wa sehemu ya maegesho ya ndege, alipotembelea kiwanja hicho mkoani Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadudu, wanyama waharibu hekari 12,000 za mazao

**Na Said Hamdani, LINDI**

HEKARI zaidi ya 12,000 za mashamba ya mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula na biashara katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, zimeharibiwa na wanyama, wadudu waharibifu wakiwamo ngedere, panya na viwavijeshi.

Wanyama wengine ni tembo, viboko ambao wamekuwa wakishambulia mazao, hali ambayo huenda ikasababisha kuwapo kwa upungufu wa chakula katika msimu wa mwaka huu.

Kaimu Ofisa Kilimo na Umwagiliaji wa Manispaa ya Lindi, Amina Pemba, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa ya uwapo wa tatizo hilo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani.

Akiwasilisha taarifa hiyo, Pemba alisema tatizo la uharibifu wa mazao ni kubwa, kutokana na wimbi la wanyama hao wakiwamo panya, ngedere wanaofukua mashimo yenye mbegu zinazopandwa. Pemba alitaja baadhi ya vijiji na kata zilizoathirika na wanyama hao ni pamoja na Mipingo, Kilolambwani, Mvuleni, Kilangara, Mnang'ole, Kitunda, pamoja na Tarafa ya Mchinga.

Alisema katika kukabiliana na tatizo hilo, Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Lindi, imeshaagiza kutoka Mkoa wa Morogoro kilo 200 na lita 1,000 za sumu kwa ajili ya kutokomeza wadudu hao.

Alisema kilo 80 kati ya 200 za viuatilifu zilizoagizwa zimewasili na kupelekwa maeneo husika.

Alisema kiasi kingine cha sumu, ikiwamo ya kuua viwavijeshi zinatarajia kuingia wakati wowote ndani ya Manispaa ya Lindi, huku akiwasisitiza wakulima kuandaa chambo kama vile pumba za mahindi na mafuta ya kula kwa ajili ya kuchanganya na sumu. Pia, aliwasisitiza wakulima kuandaa mabomba yatakayo tumika kupulizia sumu kwa ajili ya kuwanyunyuzia viwavijeshi ambao wamekuwa tishio katika kushambulia mazao mbalimbali kama vile mpunga, mahindi na mengineyo.

Baada ya maelezo hayo, madiwani waliitaka ofisi ya mkurugenzi mtendaji kuharakisha kupeleka sumu ili kunusuru nguvu za wakulima zisiendelee kupotea kwa lengo la kuepusha halmashauri yao kuingia kwenye tatizo la upungufu wa chakula.

# DC aanzisha kampeni chanjo UVIKO-19

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, Nickson Simon (Nicky wa Pili), ameanzisha kampeni maalum itakayofanyika kwa mwezi mmoja ya kutoa elimu ya kuwahamasisha wananchi wote wilayani humo kuhakikisha wanapata chanjo ya ugonjwa wa corona.

Kampeni hiyo inayojulikana kama 'Kisarawe imechanja, ujanja ni kuchanja' imelenga kuhakikisha kwamba asilimia 60 ya wananchi wanaoishi katika wilayani hiyo wanachanja na inalenga kupita katika kata zote, mtaa kwa mtaa, nyumba kwa nyumba, kupitia taasisi za dini pamoja na waelimishaji kwenye jamii, kwa kutoa elimu ya chanjo ya ugonjwa huo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkuu huyo wa Wilaya, alisema lengo la kampeni hiyo ni kuunga mkono azma kuu ya serikali ya kuhakikisha inalinda na kuwaweka salama wananchi wake dhidi ya ugonjwa huo wa corona. Alisema wanaamini kwamba endapo wananchi wakichanja upo uwezekano mkubwa wa kuwa salama dhidi ya ugonjwa huo na uhakika wa kuendelea na shughuli zao za uzalishaji mali bila hofu yoyote.

"Lengo letu kwenye wilaya hii ni kuhakikisha wananchi wote wanapata kinga madhubuti ya ugonjwa huu wa corona ili waendelee na shughuli zao za uzalishaji na kuchangia katika maendeleo ya taifa," alisema Nickson.

"Wilaya ya Kisarawe tunataka iwe ya mfano kwa wilaya nyingine kwa kuhakikisha wananchi na viongozi wake katika ngazi zote wanashiriki kikamilifu katika kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma. Tumetoa mafunzo kwa viongozi katika ngazi zote ili kuwajengea ufahamu na kuwaondolea wananchi hofu juu ya chanjo."

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Libamba Sobo, alisema wamedhamiria kufikia watu zaidi ya 40,000 katika kipindi chote cha kampeni.

"Na katika kufanikisha kampeni hii, jumla ya watoa huduma 148 wamepewa mafunzo, vijiji 84 vitafikiwa na huduma hizi katika kata 17 zilizo wilayani kwetu na tunatumia mbinu mbali mbali katika huwafikia wananchi, moja ni kupitia uhamasishaji wa mitaa na nyumba kwa nyumba, tunatumia pia taasisi za kidini pamoja na kuwatumia waelimishaji ngazi ya jamii," alisema Dk. Sobo.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la FHI360, Waziri Nyoni, alisema wamevutiwa na kampeni hiyo na kwamba wako tayari kushirikiana na uongozi wa wilaya hiyo kuifanikisha.

"Shirika letu tumevutiwa na juhudi ambazo ofisi ya mkuu wa Wilaya ya Kisarawe imezifanya katika kupambana na janga hili la ugonjwa wa corona na ndio maana tukaamua kuunga mkono juhudi hizi, na tunaahidi kuendelea kushirikiana na Wizara ya Afya na Wadau wengine katika kuhakikisha huduma na taarifa sahihi za kuhusu afya zinawafikia Watanzania wote," alisema Nyoni.

Uzinduzi wa kampeni ya chanjo ya corona wilayani Kisarawe ulienda sambamba na uchanjaji, huku baadhi ya wasanii wa muziki wa bongo fleva wakijitokeza kuongoza uchanjaji huo.

# Wapiga ramli watiwa mbaroni

**Na Christina Haule, MOROGORO**

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro linawashikilia watuhumiwa sita, wakiwamo waganga wapiga ramli chonganishi wawili wanaopotosha jamii na kuchochea matukio ya mauaji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilim, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye mdahalo wa masuala ya usalama wa wanahabari mkoa wa Morogoro na Jeshi la Polisi ulioandaliwa na Umoja wa Waandishi wa Habari mkoa wa Morogoro (MoroPC) na kufadhiliwa na Umoja wa Vilabu vya Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC).

Musilim alisema waganga hao wa jadi walikamatwa na wanaendelea kuhojiwa na polisi na watapandishwa kizimbani kwa sababu ya kuwa sehemu vya vyanzo vya mauaji kwa kupiga ramli chonganishi kutokana na kuaminiwa na jamii kwamba wana uwezo wa kumwona au kugundua mchawi.

Alivitaja vyanzo vingine vya mauaji ni ugomvi wa kifamilia kwa sababu wamebaini mauaji hayo yamekuwa hakitokea baada ya vyanzo mbalimbali katika familia, na kwamba bila kupata taarifa kwa jamii inakuwa ni vigumu kutatua migogoro hiyo, mahusiano katika ndoa na ushirikina ambapo operesheni inaendelea.

Alisema katika kukabiliana na mauaji yanayoendelea mkoani na nchini kwa ujumla, Jeshi la Polisi mkoa limetenga siku ya Alhamisi kila wiki kuzungumza na familia zenye migogoro ili kuitatua na kuzuia mauaji hayo.

Aliwashauri wanaokabiliwa na migogoro ya aina mbalimbali waende kwenye ofisi ya mkuu wa Polisi Morogoro au kwa wakuu wa upelelezi kila wilaya kujadili changamoto zao na kuzipatia ufumbuzi jambo ambalo anaamini litamaliza kasi ya matukio ya mauaji.

Kamanda Musilim alisema pia jeshi hilo limekamata watuhumiwa sita wa mauaji ambao watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Kamanda huyo alisema pia wamewakamata waendesha bodaboda sita wanaopora pochi za watu barabarani maarufu kama 'vishandu' na kusababisha watu kukosa amani mitaani.

Naye Mwezeshaji kutoka MoroPc, Idda Mushi, aliwataka wanahabari kuhakikisha wanasimamia usalama wao wawapo kazini hasa wakifuatilia habari za uchunguzi sambamba na kutoa taarifa kwa wenzao wa karibu, Jeshi la Polisi, ofisini kwao ana viongozi wa MoroPc ili uwepo ufuatilizi na kuhakikisha usalama wao mahali walipo.

Naye Ofisa Upelelezi wa makosa ya jinai mkoa wa Morogoro, Georgina Matagi, aliwashauri wanahabari kuendeleza uhusiano mzuri na jeshi hilo kwa kuandika habari zenye uwazi na ukweli.

Awali Mwenyekiti wa MoroPc, Nickson Mkilanya, alisema dhima ya mdahalo huo ni kuboresha mahusiano kati yao na Jeshi la Polisi katika utendaji kazi ili kufanya mkoa kupiga hatua kimaendelo.




Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo (wapili kulia), akimsikiliza na kumpongeza Mkurugenzi wa Chama cha Waajiri (ATE), Suzanne Ndomba-Doran, baada ya kumkabidhi vifaa vya usafi na kisha kushirikiana naye kusafisha eneo la Kiburugwa, Temeke. MPIGAPICHA WETU

# Wizi wa mifugo Bagamoyo wachosha wananchi

**Na Julieth Mkireri,**
KIWANGWA

BAADHI ya wakazi wa kijiji cha Msinune Kata ya Kiwangwa Wilaya ya Bagamoyo wamelaani vitendo vya wizi wa mifugo vinavyotokea mara kwa mara, huku wakiomba serikali kuchukua hatua zaidi kuvikomesha.

Wakizungumza na Nipashe kwa njia ya simu kwa nyakati tofauti waathirika wa matukio hayo walisema wanaohusika wamekuwa wakitoroka baada ya mifugo kupatikana, huku wanaohisiwa wakiendelea kuachwa mtaani.

Mmoja wa waathirika wa tukio la wizi lililotokea usiku wa kuamkia Februari 26, Benard Kutu, alisema alipigiwa simu usiku na kijana anayesimamia mifugo yake katika kijiji cha Msinune akielezwa kuhusiana natukio na ng'ombe wake wanane kuibwa.

Kutu alisema baada ya kupokea simu hiyo alimwelekeza kijana wake kutoa taarifa kwa viongozi wa kijiji na polisi ili hatua za kuwasaka wezi zifanyike haraka.

"Baada ya kupokea simu usiku wa saa kumi kama na dakika 20, kijana wangu aliniambia amekuta walinzi wamefungiwa ndani, huku zizi likiwa jeupe ng'ombe wote wakiwa wameibwa na watu wasiojulikana, nilimjulisha kaka yangu na mdogo wangu ili waende kunisaidia kuwasaka," alisema.

Alisema msako uliofanyika ulifanikisha ng'ombe wake kupatikana porini, lakini wezi hawakukamatwa kwani walifanikiwa kukimbia.

Mlinzi wa mifugo ya Benard, Ismail Chanzenze, alieleza kuwa majira ya saa tisa usiku alisikia mbwa wanabweka na alipotoka nje alimulikwa na tochi, lakini alifanikiwa kuwaona watu wawili jamii ya wafugaji.

Alisema baada ya kuona hali hiyo aliingia ndani kumuamsha mlinzi mwenzake aliyekuwa amelala, lakini wakati akikimbilia ndani aliwaona watu wawili wakiwa wanapiga taa kuzivunja na wengine watatu wanazunguka kwenye zizi la ng'ombe.

Ismail alisema alipoingia ndani watu hao waliendelea kupiga taa wakitumia fimbo zao, huku wakiwatishia kutulia ndani na atakayethubutu kutoka watamchoma mshale.

"Tukiwa ndani na mwenzangu tuliendelea kupiga kelele za kuomba msaada, lakini hakuna aliyetokea huku wale watu walioko nje waliendelea kutukalipia tutulie, tukiendelea na kelele zetu watavunja mlango," alisema.

Hata hivyo alibainisha kuwa baada ya muda mfupi msimamizi wao anayejulikana kwa jina la Kimungu Rajabu alifika na kuwaliza sababu za kelele walizokuwa wanapiga.

Rajabu ambaye alikuta walinzi hao wakiwa wamefungiwa kwa nje aliwafungulia mlango na walipotoka kukagua nje walikuta mifugo yote imeibwa na wezi wametokomea nayo.

Alisema walitoa taarifa kwa mmiliki wa mifugo na viongozi wengine wa kijiji na polisi ambao walifika na walinzi hao kuwekwa chini ya ulinzi hadi baadaye walipotolewa kwa dhamana baada ya mifugo kupatikana.

Hata hivyo alisema hali ya wizi wa mifugo ni tishio kwao na inaleta hofu ya kuendelea kufuga kutokana na matukio ya mara kwa mara.

Mtendaji wa Kata ya Kiwangwa, Sada Madie, alikiri kuwapo kwa matukio ya wizi katika eneo lake huku akisema hajapata taarifa ya tukio la Kijiji cha Msinune.

"Wizi wa mifugo kwenye kata yangu ni ugonjwa mkubwa tu na wanaotuhumiwa mara nyingi ni hawa (jamii ya wafugaji), ambao sio wakazi wa hapa wanakula njama na watu wa karibu wanaoiba mifugo," alisema Sada.

Alisema wamekuwa wakifanya vikao vya mara kwa mara na wananchi kuhusiana na suala hilo, lakini wapo watu wanatajwa kuhusika kula njama na wezi na watu hao wamekuwa wakionekana kwa msimu kwenye kata hiyo, na kwamba jitihada za kuwasaka wanaotuhumiwa zinaendelea.

Diwani wa Kiwangwa, Malota Kwaga alikiri kupata taarifa za mwananchi wake wa Msinune kuibiwa mifugo, na kuwa aliwaonya wananchi kuachana na tabia hiyo huku akiwataka kutoa ushirikiano kuwapata wahusika na kuepuka kujichukulia sheria mkononi.

# Expo2020 Dubai yaiweka Tanzania ramani ya dunia

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amesema maonyesho ya kibiashara ya Expo2020 Dubai yanazidi kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia kutokana na mataifa mbalimbali kufahamu Hifadhi ya Serengeti, Ngorongoro, madini ya Tanzanite, Mlima Kilimanjaro vinapatikana Tanzania na si nchi jirani.

Hatua hiyo inakuja kufuatia upotoshwaji wa muda mrefu ambao umekuwa ukifanywa na baadhi ya nchi za jirani kuwa kila vivutio vizuri vya utalii ambavyo vipo Tanzania huwahadaa watalii kuwa vipo nchini mwao.

Akizungumza na waandishi wa habari akiwa katika maonyesho hayo, Dk. Ndumbaro alisema watu mbalimbali ambao wamekuwa wakitembelea banda la Tanzania wamekuwa wakishangaa kuona madini ya Tanzanite, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Mlima Kilimanjaro pamoja na Hifadhi ya Taifa Ngorogoro kuwa zipo Tanzania.

"Nimekuwa nikizungumza na wageni mbalimbali wanaotembelea banda la Tanzania wengi wao wamekuwa wakishangaa na kukiri kuwa mwanzo walikuwa wanajua kuwa vivutio hivyo havipo Tanzania bali vipo nchi jirani," alisema Dk. Ndumbaro na kuongeza: "Maonyesho haya ya Dubai yameipaisha Tanzania kuwa ni nchi yenye utajiri mkubwa wa vivutio vya utalii ambavyo ni vizuri tofauti na wenzetu wanaopotosha kuwa ni vyao."

Miongoni mwa taasisi za Tanzania za Wizara ya Maliasili na Utalii zinazoshiriki maonyesho hayo ni Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Mamlaka ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro (NCAA), Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na Wakala wa Huduma za Misitu Tazania (TFS).

Maonyesho hayo ya kimataifa yaliyoanza Oktoba Mosi mwaka huu, yanaendelea hadi Machi 31, mwaka huu na yanashirikisha nchi zaidi ya 192.

# DC Jokate, ATE waongoza kampeni ya usafi mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE), pamoja na wanafunzi wa awamu ya saba wa programu ya mwanamke kiongozi wameshirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwogelo, kufanya usafi katika eneo la Kiburugwa wilayani humo.

Katika tukio hilo, ATE iliongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Suzanne Ndomba-Doran, pamoja na mambo mengine walikabidhi vifaaa vya kufanyia usafi kwa mkuu wa wilaya huyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Suzanne alisema: "Tumelazimika kufanya tukio hili ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kutunza mazingira na kusafisha mazingira yetu, kuunga mkono kampeni ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala iitwayo 'Safisha, Pendezesha Dar es Salaam'.

Rais wa wanafunzi wa programu ya wanawake awamu ya saba, Joyce Mgaya alisema: "Kiongozi ni yule anayatambua kuwa maendeleo yanachangiwa na usafi wa mazingira, pale mazingira yanapokuwa masafi huchagiza kuletwa kwa maendeleo kwenye jamii husika."

Aliongeza: "Sisi kama wanafunzi tunaohitimu masomo yetu ya uongozi kwa mwaka 2021-2022, tumejifunza na kutambua kuwa ili mafanikio yapatikane kwenye jamii, kiongozi unatakiwa kufanya mabadiliko na kuwagusa kuanzia wananchi wa chini, kisha matokeo yataonekana na kuleta maendeleo hadi kwa wale walioko juu."

Alisema ndiyo sababu iliyowasukuma kushirikiana na wakazi wa Kiburugwa wilayani Temeke kufanya usafi na kukabidhi vifaa vya usafi vitakavyosaidia kuendelea kutunza mazingira ya sasa na ya baadaye".

Katika kuelekea Siku ya Mwanamke Duniani, ATE imeandaa mkutano wa mwaka wa uongozi utakaofanyika Machi 2, mwaka huu wenye mada isemayo 'Usimamizi wa mabadiliko ya tabia nchi: Usawa kwa maendeleo ya sasa na baadaye.'

HABARI KITAIFA

# Tigo yapanda miti 1,000 Kilimanjaro

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya huduma za kidijitali, Tigo Tanzania imepanda miche ya miti 1,000 kama sehemu ya mradi wake unaoendelea wa Tigo Green for Kili, One Step One tree, katika mkoa wa Kilimanjaro.

Upandaji wa miche 1,000 ya miti katika kijiji cha Kwa-Sadala wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro umeanza awamu ya pili ya mradi kwa mwaka 2022.

Mradi wa Tigo Green for Kili, One Step One Tree ulizinduliwa mwishoni mwa Februari 2021, kwa lengo kuu la kuhifadhi theluji na mimea kuzunguka Mlima Kilimanjaro. Katika awamu ya kwanza, Tigo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi na ya umma ilikusanya zaidi ya miche 30,000 ya miti, lakini ilifanikiwa kupanda zaidi ya miche 11,000 ya miti.

Akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa upandaji wa miche hiyo katika eneo la Kwa-Sadala wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, Mkurugenzi wa Tigo Tanzania Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo, alisema, "Mradi wetu wa upandaji miti upo katika awamu ya pili. Tuliamua kuendelea na zoezi la upandaji miti katika msimu huu wa mvua ili miche istawi. Mwaka huu tunatarajia kupanda zaidi ya miche 20,000 ya miti ambayo itapunguza athari za ongezeko la joto duniani na kusaidia kurejesha theluji kwenye Mlima Kilimanjaro."

"Napenda kuipongeza VOEWOFO kwa kuratibu na kuandaa jambo hili adhimu, kwa sababu imekuwa si jambo jepesi, ukizingatia hali ya hewa imekuwa si nzuri kwetu, kulikuwa na ukame katika maeneo mengi ya mkoa huu, lakini mwaka huu mambo yanaonekana kuwa mazuri. , ndiyo maana tunapiga hatua kwa kupanda miche 1,000 ya miti leo."

Mkurugenzi wa Kanda ya Kaskazini wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Lewis Nzali ambaye alikuwa mgeni rasmi katika tukio hili alisema: Mradi wa upandaji miti unaofadhiliwa na Tigo Tanzania. Mradi huu wa matarajio utahakikisha Kilimanjaro ya kijani kibichi kwa miaka ijayo."

Meneja Rasilimali watu wa VOEWOFO, ambaye ni mwanachama wa Bodi ya VOEWOFO, Neema Mahimbo, aliipongeza Tigo kwa kuendeleza mradi wake wa kuhifadhi mimea inayozunguka Mlima Kilimanjaro. "Tunatarajia kuendelea kufanya kazi na Tigo na wadau wengine, tunaporejesha mradi huu. Tunaamini kwamba kwa msaada wa Tigo, tuko karibu zaidi kufikia lengo letu na kuchangia Kilimanjaro yenye kijani kibichi kwa vizazi vijavyo."

# Waandishi wa habari wafunzwa umuhimu wa sera ya mazingira

**Na Christina Mwakangale**

WAANDISHI wa habari pamoja na wadau wa sayansi na teknolojia, wameelezwa umuhimu wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021, kwamba itapanua wigo na fursa za kibiashara zitokanazo na mazingira nchini.

Mkurugenzi wa Uratibu na Usimamizi Uendelezaji wa Utafiti, Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Bugwesa Katale, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam kwenye mafunzo, kuwajengea uwezo wadau hao kuhusu sera mpya.

Alisema sera mpya ilizinduliwa Februari, mwaka huu na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, ambayo inalenga kuondoa mapungufu, vikwazo na changamoto zilizokuwamo kwenye Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997.

"Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 ilikuwa na changamoto ya kukosekana kwa baadhi ya masuala hasa kipindi cha Uviko-19, kwa sababu sera hii haikutoa miongozo inayotakiwa kutumika kwenye sekta kadhaa.


"Sera mpya imeboresha maeneo kadhaa na kuongeza fursa na kuruhusu matumizi ya teknolojia ya uhandisi jeni (Biotechnology) katika kilimo, afya na viwandani," alisema Dk. Katale.

Akiwasilisha mada kuhusu ubunifu katika teknolojia ya uhandisi jeni, Thomas Chali, kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, alisema baada ya sera kuzinduliwa Februari, mwaka huu, mwongozo umetolewa kuhusu teknolojia hiyo ikiwamo ulinzi wa mazingira.

Chali alisema changamoto zilizokuwamo kwenye Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997, ni pamoja na kukosekana mwongozo wa mabadiliko ya tabianchi, udhibiti wa taka ngumu, wadudu vamizi na matumizi ya uhandisi jeni ili kutengeneza dawa.

"Ongezeko la maisha ya kisasa, mwingiliano wa watu eneo moja hadi lingine inasababisha uharibifu wa mazingira. Matumizi mapya ya mbegu, bidhaa za kiteknolojia kuongezeka ikiwamo simu, televisheni kumeongeza uchaguzi na tatizo la kudhibiti taka zake," alisema Chali. Alisema sera mpya imeibua fursa mbalimbali ikiwamo taka kubadilishwa kuwa biashara akitolea mfano bidhaa plastiki na chuma, zimeibua soko la chuma chakavu na urejelezwaji wa taka za plastiki viwandani.

"Awali sera haikuzingatia fursa katika mazingira. Sasa taka zilizoonekana kama tatizo ni fursa kibiashara, watu hivi sasa wanaokota makopo, chupa na kuuza, zamani watu hawa jamii iliwatafsiri kama vichaa, wendawazimu. Mtazamo kijamii umebadilika inaonekana shughuli hiyo ni ajira," aliongeza Chali.



Mkuu wa Sekta ya Kilimo Kitengo cha Uwekezaji Benki ya Stanbic, Henry Kapungu (watatu kushoto), akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa TPC Ltd, Marius Jacobs (wanne kulia), mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 19, kwa niaba ya FT Kilimanjaro, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya Shule ya Sekondari ya Katanini iliyoko Kata ya Kindi, wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro. Wengine ni wafanyakazi wa Stanbic na mwakilishi kutoka FT Kilimanjaro. **MPIGAPICHA WETU**

# CNG kuwainua kiuchumi madereva Bolt

**Na Jenifer Gilla**

KAMPUNI ya usafirishaji wa abiria ya Bolt imeanza kampeni ya kuwahimiza madereva kutumia gesi iliyochakatwa kwa mfumo asilia 'Compressed Natural Gases' (CNG) katika vyombo vya moto, ambayo inatajwa kupunguza gharama na kutunza mazingira.

Meneja wa Bolt nchini, Remmy Eseka, alisema lengo kuu la matumizi ya nishati hiyo ni kulinda mazingira ili kuwa na miji bora huku wakiwawezesha madereva kuongeza kipato kwa kutumia gesi yenye bei nafuu.

Alisema gesi hiyo ni salama kuliko petroli na dizeli, na inapunguza utoaji wa kaboni kwa asilimia 90 hadi 9, hutumiwa katika magari ya jadi ya petrol na injini ambazo zimerekebishwa au zimetengenezwa mahususi kwa matumizi ya CNG.

Alisema Bolt inaendelea kuwekeza kwa dhati katika katika sekta ya usafiri kote barani Afrika na inataka kupanua njia mbadala za kuwapa huduma bora wateja wake, huduma hizo zitajumuisha kitengo cha wapanda farasi wa Bolt na baiskeli za kielektroniki.

Amri Mkiwa, dereva wa Bolt anayetumia nishati hiyo kwa miaka miwili sasa, aliisifia kuwa ni ya gharama nafuu ukilinganisha na nishati nyingine kama petroli.

Anasema kuwa tangu ameanza kutumia gesi hiyo asili ameona tofauti kubwa ikiwamo kuongezeka kwa kipato chake tofauti na hapo awali. "Tangu nianze kutumia gesi ya CNG kipato changu kama dereva kimeongezeka kwa kupitia kwa asilimia 85 kwani gharama kubwa za awali zimepungua," alisema.

Aliongeza kuwa sasa anatumia Sh. 15,000 kujaza gesi, tofauti na hapo awali alipokuwa akitumia Sh. 30,000 hadi 35,000 kujaza petrol ambayo haikai muda mrefu.

Mtumiaji mwingine wa gesi hiyo, Elias Mruma, alisema nishati hiyo ni rafiki wa mazingira ikiwa mchanganyiko wa asilimia moja ya methanol katika ujazo wake.

"Tangu nimeanza kutumia gesi ya CNG, nimepunguza gharama na kuongeza faida iliyonisaidia kupeleka watoto wangu wawili katika shule za kimataifa," alisema na kuongeza:

"Kiwango cha juu kabisa ninachotumia ni kujaza gezi ni Sh. 17,500 na kuniwezesha kupata angalau Sh. 70,000 kwa siku nikitumia jukwaa la Bolt."

Alifafanua kuwa matumizi ya gesi asilia yanasaidia kupunguza gharama za mtu hadi asilimia 75.

# Shule Kilosa zasaidiwa viti, meza na madawati

**Na Mwandishi Wetu**

SHILE mbili wilayani Kilosa mkoani Morogoro zimepatiwa msaada wa vifaa mbalimbali vya elimu.

Shule zilizonufaika kwa msaada huo uliotolewa na Benki ya NMB ni Shule ya Msingi Kilosa Town na Shule ya Sekondari Lumuma ukijumuisha viti na meza 50 na madawati 50 vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 10.

Utoaji wa msaada huo ulifanyika wakati wa uzinduzi wa tawi la NMB wa huduma za benki inayotembea katika mji mdogo wa Dumila ukiwa ni mchakato kwa benki hiyo ya kujiandaa kwa ajili ya kujenga tawi kubwa kutokana na mji huo kuwa na majukumu ya kibiashara mkoani Morogoro.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema wananchi wa Dumila waliokuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma za kibenki ya benki hiyo sasa wataondokana na adha hiyo.

Mlozi alisema wakazi wa Dumila na vijiji vya jirani walikuwa wakipata shida kufikia na kupata huduma kutoka taasisi za kibenki.

Alisema Dumila ni mji wenye shughuli nyingi za kimaendeleo na wananchi wake wanaendesha shughuli nyingi za kiuchumi za kilimo, ufugaji, madini na kukosekana kwa taasisi ya kibenki ndio sababu ya kuendelea kujitanua kwa kuzindua tawi la benki ya hiyo.

Mlozi alisema benki hiyo imekuwa ikiisapoti serikali kwa wananchi kwa kutoa msaada kwa vifaa katika sekta ya elimu, afya, elimu ya utunzaji bora wa fedha na eneo la majanga ni sehemu wamekuwa kusaidia jamii wanaopata majanga.

Mkazi wa Dumila, Hawa Mohamed, alisema sasa wananchi wa mji huo wataondokana na adha ya kutembea umbali mrefu waliokuwa wakifuata huduma za kibenki kutoka Dumila hadi Turiani kilometa 50, Dumila hadi Kilosa kilometa 60 na Dumila hadi Mvomero kilometa 20 ambapo kuna matawi ya benki hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Abdu Majid Mwanga, alisema Dumila imekuwa na kilio cha muda mrefu wa uhitaji wa matawi ya benki na ufunguzi wa tawi la Benki ya NMB inaenda kuondoa changamoto ya wananchi waliokuwa wakitembea umbali mrefu kwenda Kilosa, Turiani na Morogoro.



Meneja Uhusiano wa Benki ya Absa Tanzania, Linda Lance (kulia), akipata vipimo kabla ya kujitolea damu kwa ajili ya kusaidia wodi mpya ya wazazi katika Hospitali ya CCBRT jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Ofisa Muuguzi wa Hospitali ya CCBRT, Christina Baluhya na Fundi Sanifu wa Maabara ya Hospitali hiyo, Athumani Daffa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Agizo halmashauri, TADB kuwezesha vikundi ushirika

**Na Mbaraka Kambona**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameziagiza halmashauri hususan zilizoko katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi kutoa asilimia 10 zinazotengwa na serikali kwa ajili ya kuwezesha vijana na kuwapa vikundi vya ushirika vya wafugaji.

Wafugaji hao ni wa jongoo bahari, kaa na wakulima wa mwani ili waweze kuongeza nguvu na kuendeleza shughuli zao za uzalishaji.

Ulega alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwa nyakati tofauti na wanavikundi wa ufugaji majongoo bahari na ukulima wa mwani alipowatembelea kukagua shughuli wanazofanya wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kupitia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Shauri Selenda, kuwa asilimia 10 zinazotengwa na serikali kwa ajili ya kuwezesha vijana wapewe wanavikundi hao wanaofuga jongoo bahari, kaa na kilimo cha mwani ili waweze kufanya uzalishaji mkubwa na wenye tija.

"Tunataka hii Pwani yetu yote kuanzia Moa kule Tanga mpaka Msimbati itumike kwa ajili ya shughuli za uzalishaji, vijana na kinamama wawezeshwe kufanya shughuli hizi ili kuvutia watu wengine kufanya shughuli hizi na kuzalisha kwa tija zaidi," alisisitiza Ulega. Alisema lengo la kuwezesha vikundi hivyo ni kutaka wakue ili watoke katika uzalishaji mdogo na kuwa Kampuni na kuzalisha kwa wingi kitendo ambacho kitawaongezea kipato wao na taifa kwa ujumla.

"Haya mambo mnayofanya ya uzalishaji yameandikwa katika ilani ya Chama Cha Mapinduzi, na hizo pesa tunazosema zitolewe ni utekelezaji wake chini ya maono ya Rais Samia Suluhu Hassan," alifafanua.

Aidha, Ulega aliutaka uongozi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kutembelea vikundi hivyo ili kujua changamoto zao na kuwaelekeza namna ya kufanya ili waweze kukopeshwa na benki hiyo.

"Lakini natoa maelekezo pia kwa watu wa Benki ya Kilimo, mtembelee hivi vikundi mpange vizuri na muwaongezee nguvu ili wapate mavuno ya uhakika, wewe Afisa Biashara kutoka Benki ya TADB, nakupa wiki moja urudi hapa ukutane na hawa wanavikundi, uweke nao mikakati na uwaelekeze namna ya kufanya ili waweze kupata hiyo mikopo",alisema

Aliwahimiza vijana kuendelea kuchangamkia fursa hizo za ufugaji wa majongoo bahari na ukulima wa mwani kwa sababu soko biashara hiyo ina manufaa makubwa na soko pana ambalo sio rahisi kulikidhi.

Katika hatua nyingine, Ulega pia alivipongeza vyombo vya habari kwa kazi nzuri wanayofanya ya kutangaza vyema fursa mbalimbali zinazopatikana katika uchumi wa buluu na hivyo aliendelea kuwaomba kuendelea na kazi hiyo ya kutangaza fursa hizo zinazopatikana nchini ili ziweze kuvutia wawekezaji wengi zaidi.

Lengo la ziara yake mkoani Pwani ni kutathmini na kufanya kikao kazi cha kuweka mikakati na kampeni ya kuhamasisha kutumia ipasavyo fursa za uchumi wa buluu huku akisisitiza kuwa baada ya miezi mitatu atarejea tena katika maeneo hayo ili kufanya ufuatiliaji wa maelekezo hayo.

# Wasichana kuendelea kuhamasishwa sayansi

**Na Mwandishi Wetu**

ILI kuhakikisha vijana wengi zaidi wa kike nchini wanasoma masomo ya sayansi, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) imesema itaendelea kuwahamasisha kupenda na kusoma fani mbalimbali za sayansi kupitia programu yake inayojulikana kama STEM.

STEM ni programu inayoendeshwa na kampuni ya SBL ambayo huwachukua kutoka vyuoni vijana wa kike wanaofanya vizuri katika fani za sayansi, teknolojia pamoja na hisabati na kuwapa fursa ya kujifunza kwa vitendo kwa muda wa mwaka mmoja katika viwanda vyake.

Akizungumza na gazeti hili, mratibu wa programu hiyo, Saraphina Mwamaso, alisema SBL ilianzisha programu hiyo mwaka 2020 ikilenga kuwahamasisha vijana wa kike kusoma masomo ya sayansi kwa kuwapa fursa ya kujifunza kwa vitendo zaidi. "Tangu tuanzishe programu hiii mwaka 2020, vijana wengi wa kile wameweza kupata fursa ya kujifunza kwa vitendo katika idara zetu mbali mbali. Lengo letu ni kuona mtoto wa kike anakuwa sehemu ya maendeleo y sayansi kwa kunufaika moja kwa moja na fursa mbalimbali," alisema.

Mtaribu huyo anasema STEM huwaweka chini ya uangalizi maalum ambapo wanaufaika hupata fursa ya kujifunza na kufundishwa mambo tofauti toafuti yanayowasaidia kuendeleza na kukuza vipaji katika taaluma zao," alisema.

Lydia Masonda, mmoja wa wanufaika wa programu hiyo ambaye amesomea sayansi ya chakula na teknolojia kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), anasema ni jambo la muhimu kutambua uwezo na ushiriki wa vijana wa kike katika sayansi ili kuwatia moyo na kuwapa ari zaidi ya kuwa katika fani hizo "Fursa wanayotoa SBL kwa sisi vijana wa kike kupitia STEM ni jambo zuri sana. Binafsi, kupata fursa hii kumenifanya nione nilifanya chaguo sahihi kuwa katika fani ya sayansi," alisema

Catherine Kagengere, kutoka Chuo cha Teknalojia Dar es Salaam (DIT), alisema: "Mimi nafikiri ili kuweza kuziba pengo la ushiriki mdogo wa vijana wa kike katika fani za sayansi ni muhimu sisi wenyewe kuamini kuwa tunaweza. Ni lazima tuepukane na mtizamo kuwa sisi ni dhaifu tukilinganishwa na wanaume." Catherinre alitoa wito kwa vijana wa kike kuingia katika fani za sayansi billa woga, "kama mimi nisingefanya hivyo nisingeweza kufanya kazi katika kampuni kubwa kama SBL."

Nipashe
# Spotika



KIKOSI CHA KWANZA CHENYE ASISTI NYINGI EPL MSIMU HUU UK. 12 - 13




ARSENAL

# TIMU TANO ZENYE WACHEZAJI VIJANA ZAIDI LIGI KUU YA EPL

**LONDON,** Uingereza

LIGI Kuu England (EPL), inajivunia kutoa baadhi ya chipukizi wenye vipaji barani Ulaya. Nyota hawa wanaweza kuwa bado wanajifunza, lakini ndio mustakabali wa klabu zao na wanaweza kuendelea kutengeneza historia.

Baadhi ya makocha wamewageukia vijana wao msimu huu, wakiweka imani kwa vijana na kukirekebisha kikosi. Wachezaji kuondoka na kustaafu ni sehemu ya ukuaji wa klabu. Mtu hawezi kupata kila mara mchezaji mwenye uzoefu mkubwa katika soko la uhamisho, na ni kazi ya kocha kutoa mafunzo na kukuza vipaji vijavyo.

Timu nyingi za Ligi Kuu England zimebarikiwa kuwa na furaha ya ujana, ambayo ni ulinzi kwa mustakabali wao. Shauku na cheche walizonazo vijana hawa imekuwa jambo la kuburudisha kwa mashabiki kote ulimwenguni.

Sasa makala haya yanaviangalia vikosi vitano vya Ligi Kuu England ambavyo vina wachezaji wengi zaidi vijana...

### #5. LEEDS UNITED – WASTANI MIAKA 25.4

Huu ni mchujo wa pili kwa Leeds United kwenye Ligi Kuu tangu kupanda daraja mwanzoni mwa msimu wa 2020-21. Ingawa wako katika nafasi mbaya zaidi ya msimu uliopita, Leeds bado wanafurahisha kuwatazama. Mtindo wao wa uchezaji wa kasi ya juu na uchezaji wao mkali umezisumbua hata klabu kubwa za Ligi Kuu.

Falsafa ya kushambulia ya kocha Marcelo Bielsa imekita mizizi katika kikosi cha Leeds, ambacho ni kichanga, na wastani wao wa umri ni miaka 25.4. Joe Gelhardt na Charlie Cresswell, wote wenye umri wa miaka 19, ndio wachezaji wachanga zaidi kwenye timu hiyo.

Gelhardt ndiye anaongoza kwa kutoa asisti kwa Leeds akiwa na tatu hadi sasa. Golikipa, Kipa Ian Meslier mwenye umri wa miaka 21, ndiye mfungaji wa mashuti mdogo zaidi kwenye ligi.

Leeds wamefanikiwa kushinda michezo mitatu pekee kati ya 10 iliyopita ya ligi na kwa sasa wako nafasi ya 15 kwenye msimamo.

### #4. SOUTHAMPTON – WASTANI MIAKA 25.3

Southampton daima imekuwa ikijulikana kwa kukuza vipaji vya chipukizi. Hata hivyo, wengi wa wachezaji hawa waliondoka ili kuendeleza kazi zao mbele. Sadio Mane, Luke Shaw, na Gareth Bale ni baadhi tu ya nyota ambao wamekuwa sehemu ya kikosi cha 'Watakatifu' hao siku za nyuma.

Wastani wa umri wa kikosi hiki ni miaka 25.3. Tino Livramento mwenye umri wa miaka 19, ambaye amekuwa mmoja wa chipukizi bora zaidi kwenye ligi msimu huu, ndiye mchezaji mchanga zaidi kwao. Mwingereza huyo alisajiliwa na Southampton kutoka Chelsea Agosti 2021 kwa ada ya pauni milioni 5. Armando Broja mwenye miaka 20, yuko kwa mkopo kutoka Chelsea na ndiye mfungaji bora wa pamoja wa Southampton akiwa na mabao sita ya Ligi Kuu.

Southampton wamekuwa na mechi tatu za mwisho za kipekee kwenye Ligi Kuu. Walitoka sare dhidi ya Manchester City na Manchester United na kunyakua pointi zote tatu dhidi ya Tottenham Hotspur. Pia wako katika raundi ya tano ya Kombe la FA, ambapo watamenyana na West Ham United.

### #3. NORWICH CITY – WASTANI MIAKA 25.3

Kurejea kwa Norwich City kwenye Ligi Kuu msimu huu hakujaenda kulingana na mpango. Wametatizika kuendana na mechi zilizosalia za ligi na kwa sasa wako nafasi ya 20 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kama vile Southampton, Norwich pia wana kikosi cha wastani wa umri wa miaka 25.3. Andrew Omobamidele mwenye miaka 19, ndiye mchezaji mwenye umri mdogo zaidi katika kikosi hicho. Wachezaji waliosajiliwa majira ya kiangazi Billy Gilmour, Ozan Kabak, Josh Sargent, na Brandon Williams, ambao wote wako chini ya miaka 21, wamekuwa sehemu muhimu ya kikosi cha Norwich msimu huu.

Norwich City wameshinda mechi nne pekee za Ligi Kuu hadi sasa na kupoteza 17.

### #2. BRENTFORD – WASTANI MIAKA 25

Brentford ilijitangaza kwenye Ligi baada ya kupanda daraja kwa mtindo wa kuvutia kwa kuifunga Arsenal mabao 2-0 siku ya ufunguzi wa Ligi Kuu. Vijana hao wa kocha, Thomas Frank walionekana kuwa tishio zaidi kwenye mchezo huo wa ufunguzi.

'Nyuki' hao wana wastani wa umri wa kikosi wa miaka 25. Fin Stevens mwenye umri wa miaka 18, ndiye mchezaji mdogo zaidi wa Brentford. Hata hivyo, amecheza katika mechi nne pekee katika mashindano yote msimu huu. Bryan Mbuemo mwenye umri wa miaka 22, amekuwa chipukizi bora wa Nyuki hao msimu huu. Ana mabao matatu na anaongoza chati kwenye asisti akiwa na pasi za mwisho tatu hadi sasa.

Baada ya kuanza vema msimu wa Ligi Kuu, Brentford wanaonekana kuishiwa nguvu. Wameshinda michezo miwili pekee kati ya 10 iliyopita ya ligi na kwa sasa wako nafasi ya 14.

### #1. ARSENAL – WASTANI MIAKA 24.2


Baada ya kuanza vibaya msimu wa Ligi Kuu England, meli ya Arsenal inaonekana kuimarika. 'Washikabunduki' hao wanaonekana kuwa thabiti zaidi kwa sasa, haswa katika suala la ulinzi. Wamekuwa na historia ya kutocheza vizuri kwenye safu ya ulinzi, lakini msimu huu umeonekana kuwa bora.

Arsenal wanajivunia kuwa na kikosi cha vijana zaidi kwenye ligi, wakiwa na wastani wa umri wa miaka 24.2. Kocha Mikel Arteta ameweka imani yake kwa vijana wake. Bukayo Saka na Gabriel Martinelli wote wenye miaka 20 ndio wachezaji wachanga zaidi kwenye kikosi cha Arsenal. Wawili hao wamekuwa bora, hadi sasa wakiwa wamefunga mabao 10 na pasi za mabao sita kati yao kwenye ligi.

Emile Smith Rowe (21), Martin Odegaard (23), na Aaron Ramsdale (23) pia wamekuwa nyota bora. Arsenal kwa sasa wako nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi, lakini wamecheza mechi tatu pungufu kuliko Manchester United, ambao wako juu yao wakiwazidi kwa pointi mbili pekee.

## ISIKUPITE

NYOTA wa zamani wa timu ya Taifa ya Brazil, Ronaldo Luis Nazário de Lima, ndiye mchezaji pekee hadi sasa anayeshikilia rekodi ya kutwaa tuzo Ballon d'Or akiwa na umri mdogo zaidi baada ya kuitwaa kwa mara ya kwanza mwaka 1997 wakati huo akiwa na miaka 21.



# KIKOSI CHA KWANZA CHENYE ASISTI NYINGI EPL MSIMU HUU

**LONDON,** England

LIGI Kuu England (EPL), imekuwa ikiendelea kuwa ya kuburudisha zaidi. Wakati Manchester City wanaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri katika mbio za ubingwa, bado kuna mengi ya kushuhudia kwenye mbio nne bora na vita vya kushuka daraja.

**Hebu sasa tuangalie kikosi cha kwanza (first 11), chenye pasi za mwisho (asists) nyingi ya pasi za mabao kwenye ligi. Mfumo ulioangaliwa ni ule wa 4-3-3, haya sasa...**

### GOLIKIPA: JOSE SA

Mlinda mlango wa Wolverhampton Wanderers, Jose Sa, amekuwa mmoja wa wachezaji waliofanya vizuri kwenye Ligi Kuu England msimu huu. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno amekuwa imara zaidi langoni, akiokoa hatari nyingi.

Sa, pasi yake ya bao msimu huu ilipatikana kwenye mchezo dhidi ya Southampton Septemba 2021. Pasi ya mlinda mlango huyo ilimkuta kwa uzuri Raul Jimenez, ambaye alimalizia kwa ustadi na kufunga bao.

Sa amekuwa kipa wa kwanza wa Wolves kutoa asisti kwenye ligi tangu, Wayne Hennessey Oktoba 2009.

Wolves wamekuwa na safu imara ya ulinzi msimu huu, wameruhusu mabao 17 pekee. Vinara wa Ligi Manchester City, ambao wameruhusu mabao 14, ndio timu pekee iliyo na rekodi bora ya safu ya ulinzi.

### BEKI WA KULIA: TRENT ALEXANDER-ARNOLD

Hakuna mtu atakayeshangaa kuona Trent Alexander-Arnold kwenye orodha hii. Mwingereza huyu amekuwa mchezaji bora wa Liverpool, akitengeneza nafasi nyingi kutoka upande wa kulia.

Katika misimu michache iliyopita, Alexander-Arnold amejidhihirisha kuwa mmoja wa mabeki bora wa kulia barani Ulaya. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kwa sasa anaongoza kwenye viwango vya ligi kwa kutoa pasi za mabao 10 hadi sasa.

Akiwa ni zao la akademi ya vijana ya Liverpool, Alexander Arnold amekuwa kipenzi cha mashabiki. Mwingereza huyo tayari ana mataji manne, likiwamo la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu.

### BEKI WA KATI: ANTONIO RUDIGER

Antonio Rudiger amekuwa na msimu wa aina yake kwenye Ligi Kuu England. Mjerumani huyo ni mmoja wa mabeki bora wa kati kwenye ligi hiyo.

Michango ya Rudiger ilikuwa nguzo muhimu kwa Chelsea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, amefunga mabao mawili na kusaidia mengine wawili kufikia sasa. Amekosa mechi moja pekee kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Mkataba wa Rudiger unamalizika mwishoni mwa msimu huu na inasemekana hajapanga kuongezwa tena na Chelsea. Real Madrid, Bayern Munich na PSG wanasemekana kuwa wanamwania beki huyo.

### BEKI WA KATI: RUBEN DIAS

Ruben Dias amekuwa beki bora wa kati wa Manchester City na ameziba vyema pengo la Vincent Kompany aliyeondoka mwaka 2020.

Mreno huyo ni mtu muhimu ndani na nje ya uwanja na ameibuka kama kiongozi mwenye hamasa katika chumba cha kubadilishia nguo.

Mbali na kuwa beki bora, Dias ni bora na ana ustadi wa kucheza kutoka nyuma. Dias ametoa pasi tatu za mabao katika msimu huu wa Ligi Kuu.

Man City ilimsajili Dias katika dirisha la uhamisho wa majira ya joto la mwaka 2020, na kulipa Benfica ada ya pauni milioni 65 kwa beki huyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alishinda taji la ligi akiwa na City msimu uliopita na pia aliteuliwa kuwa Mchezaji Bora wa Ligi Kuu wa safu ya ulinzi.

### BEKI WA KUSHOTO: ANDREW ROBERTSON

Andrew Robertson amekuwa mchezaji anayetegemewa kwenye safu ya kushoto ya Liverpool tangu aliposajiliwa tena mwaka wa 2017. Robertson ana uhusiano mzuri na Trent Alexander Arnold, na wawili hao wanaushirikiano mzuri zaidi.

Robertson sasa amekuwa mmoja wa mabeki bora wa kushoto kwenye ligi. Raia huyo wa Scotland ana asisti nane kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 ana pasi za mabao 47 za Ligi Kuu katika maisha yake ya ligi, akiwa amepungukiwa sita tu na Leighton Baines, ambaye ana rekodi ya sasa ya kutoa pasi nyingi zaidi(53) kwa mlinzi wa EPL.


ALEXANDER-ARNOLD

### KIUNGO WA KATI: PAUL POGBA

Paul Pogba alianza msimu wa Ligi Kuu kwa kiwango bora kabisa. Mfaransa huyo alikuwa katika kiwango cha juu na alitoa asisti saba katika mechi zake nne za kwanza. Mashabiki wa Manchester United walifurahi sana kumwona Pogba akiwa katika ubora wake mzuri.

Hata hivyo, Mfaransa huyo alipata jeraha ambalo halikutarajiwa wakati akiwa kwenye majukumu ya kitaifa Novemba na ilimbidi kukosa mechi 11 za Ligi Kuu.

Alirejea uwanjani mapema mwezi huu, akifunga bao zuri dhidi ya Burnley. Pogba ana asisti nane kwenye ligi msimu huu.

Hakuna ubishi kwamba Pogba anaifanya United kuwa timu bora na mashabiki watatumaini kuwa anaweza kucheza sehemu muhimu katika kipindi kilichosalia cha msimu.

Man United kwa sasa wako nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi, lakini wanaweza kuteremka hadi nafasi ya sita ikiwa Tottenham na Arsenal watashinda michezo yao miwili ya mkononi.

### KIUNGO WA KATI: MASON MOUNT

Mason Mount anaishi katika ndoto ya klabu yake ya utotoni. Amekuwa mmoja wa wahitimu bora ambao akademi ya 'Blues' imewatoa hivi karibuni, akikua kwa kasi na kuwa kiungo wa kiwango cha kimataifa na kipaji chake cha ajabu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amekuwa mtu muhimu kwa kocha Thomas Tuchel msimu huu. Huku Romelu Lukaku na Werner wakionekana kutokuwa kwenye ubora wao.

Mount amekuwa mmoja wa wachezaji bora wa Chelsea kwenye Ligi Kuu na anaongoza katika chati za ufungaji na pasi za mabao. Ana mabao saba na asisti sita kwenye ligi hadi sasa.

Mount amepata mafanikio makubwa sana katika umri mdogo kama huo. Mwingereza huyo alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Chelsea msimu uliopita na alikuwa sehemu ya mafanikio yao ya hivi majuzi katika Kombe la Klabu Bingwa Dunia.

### KIUNGO WA KATI: BRUNO FERNANDES

Ni wachezaji wachache waliosajiliwa msimu wa baridi wameleta matokeo kwenye Ligi Kuu England kama Bruno Fernandes.

Fernandes alisajiliwa Manchester United Januari 2020 kutoka Benfica kwa ada ya awali ya pauni milioni 46.6.

Fernandes ana asisti tano msimu huu. Mateo Kovacic pia ana asisti tano, lakini Mreno huyo alichaguliwa hapa kwani alifunga mabao zaidi (8) na kuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye timu.

Bruno anashika nafasi ya pili kwenye chati za Man United kwa wafungaji mabao, nyuma ya Cristiano Ronaldo, ambaye amefunga mabao tisa ya ligi.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 amekuwa na wakati mgumu kwenye Ligi Kuu msimu huu. Mashabiki watatumaini Fernandes anaweza kurudia kwenye kiwango chake kama iliyvokuwa msimu uliopita ambao alifunga mabao 18 na kutoa asisti 11.

### WINGA WA KULIA: MOHAMED SALAH

Mohamed Salah bila shaka amekuwa mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu msimu huu. Mmisri huyo anaonekana kufunga kwa kujifurahisha na pia ametengeneza nafasi nyingi kwa wachezaji wenzake.

Takwimu za Salah ni za kushangaza ikizingatiwa kwamba, amekosa kucheza kwenye ligi kwa wiki chache kutokana na Kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON.

Salah ana asisti tisa za Ligi Kuu msimu huu, ambayo ni ya pili kwa ubora kwenye ligi. Yeye yuko nyuma ya Alexander-Arnold aliyetajwa hapo juu. Akiwa na mabao 16, Salah pia kwa sasa anaongoza mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu ya England.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, aliachwa na huzuni baada ya kumalizika vibaya kwenye fainali ya AFCON. Misri ilipoteza kwa mikwaju ya penalti 4-2, na mchezaji mwenzake wa Liverpool, Sadio Mane alitwaa ubingwa akiwa na Senegal.

### WINGA WA KUSHOTO: NATHAN REDMOND

Nathan Redmond alisajiliwa Southampton mwaka 2016 na amekuwa mmoja wa wachezaji bora wa 'Watakatifu' hao. Muingereza huyo alikuwa na msimu wa kuvutia sana wa 2018-19 ambapo alitajwa kuwa Mchezaji Bora wa Msimu wa Southampton wa mashabiki na wachezaji.

Redmond ana asisti tano kwenye ligi msimu huu. Amekuwa mtu muhimu kwa Southampton. Redmond amekosa mechi kadhaa zilizopita baada ya kupata jeraha kabla ya Southampton kushinda mabao 3-2 dhidi ya Tottenham.

Kocha Ralph Hassenhutl alithibitisha kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amerejea mazoezini. Southampton wako katika hali nzuri, wakivuna pointi dhidi ya City, Tottenham na United.

Kwa sasa wako katika nafasi ya tisa kwenye ligi, lakini wanaweza kumaliza msimu kwa kiwango cha juu ikiwa wataendelea katika kiwango chao cha sasa.

### STRAIKA: GABRIEL JESUS

Gabriel Jesus amekuwa na Manchester City kwa zaidi ya miaka mitano na amekuwa tishio katika safu yao ya ushambuliaji. Mbrazil huyo alijiunga na City akitokea Palmeiras mwaka 2017, lakini mara nyingi alikuwa akizidiwa na Sergio Aguero.

Hata hivyo, Jesus ametoa mchango mkubwa chini ya Kocha Pep Guardiola.

Mbrazil huyo ana asisti saba katika msimu wa sasa wa Ligi Kuu. Jesus amekosa mechi nne za mwisho za City kutokana na jeraha la misuli. Uwezo mwingi wa Jesus umekuwa baraka kwa Guardiola, ambaye amemsifu nyota huyo mwenye umri wa miaka 24.

Wako kileleni mwa Ligi Kuu, wakifuatiwa kwa karibu na Liverpool, ambao wako nyuma kwa pointi sita wakiwa na mechi moja mkononi.

## Nukuu

"Ni mchezaji mwenye ubinafsi - Ronaldo ni kuhusu Ronaldo. Ikiwa hatafunga, hatafurahi. Tuliona pale Juventus wakati, baada ya kuondoka, Giorgio Chiellini alisema wanaweza kuwa familia tena. Inapaswa kuwa kuhusu Manchester United na timu, lakini imekuwa huhusu yeye, na sasa tunaona kufadhaika kamili," **Mchezaji wa zamani wa Manchester United, Paul Ince akizungumzia ubinafsi wa Cristiano Ronaldo uwanjani.**



"Binafsi, uhusiano unakuwa mkubwa wakati kila mmoja anapoonyesha heshima na kamwe kwenye hilo sijawahi kumwangusha mtu, kwa sasa [Gareth] Bale haonyeshi morali yoyote, lakini anataka kumaliza mambo yake hapa kwa njia nzuri. Bale ameisaidia klabu hii kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, Copa del Rey na sasa muda wake umefikia mwisho," **Kocha Mkuu wa Real Madrid, Carlo Ancelotti.**



"Ukweli ni kwamba nilizaliwa Madrid, lakini mwisho wa siku ni jiji tu, sasa najihisi kama ninatokea Manchester, najihisi kama yeyote anayetokea Manchester sehemu unapopendwa ulipokaribishwa kama nyumbani kwako. Sijioni nikiondoka Manchester United, nipo hapa kwa miaka najua chochote kinaweza kutokea kwenye maisha lakini sioni nikiondoka," **Kipa wa Man United, David de Gea.**



SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Mpangaji** atuhumiwa kuuza nyumba ya mmiliki mil. 140/-

UKURASA 4



KIKOSI CHA KWANZA CHENYE ASISTI NYINGI EPL

UKURASA 12

Nipashe
Jumatatu Februari 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580870
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Washtakiwa ugaidi wapewa dhamana

• **Mchungaji** matatani tuhuma usafirishaji binadamu... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### RADI ILIVYOUA WATU SABA, KUJERUHI 14

WATU saba wamekufa kwa kupigwa na radi katika matukio mawili tofauti yaliyotokea katika Kijiji cha Milundikwa Kata ya Nkandasi wilayani Nkasi...

UKURASA WA 3

### 12 WAHOFIWA KUFA AJALI NDEGE YA Z'BAR

WATU 12 wanahofiwa kufariki baada ya ndege ya Kampuni ya Flyin Zanzibar yenye namba SH-MZA kuanguka baharini katika kisiwa...

UKURASA WA 4

### CHADEMA KUNUSURU MAKADA WALIOFUNGWA

ZIKIWA zimepita wiki mbili tangu wanachama wanne wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kata ya Majengo, Halmashauri ya...

## Watanzania waelekezwa pa kukimbilia vita Ukraine

UKURASA 3



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Dk. Ahmed Jaylan ambaye ni Kiongozi wa Ujumbe wa Muslim World League nchini Saudi Arabia, alipotembelea maonyesho ya kongamano la elimu ya dini, lililofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Rais Samia ashuhudia utiaji saini mikataba 36 ya tril. 17/-

UKURASA 2

**MICHEZO** **KASEJA, KOCHA WATOA SIRI USHINDI** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6




MAKATA

# MAKOCHA 10 WALIVYOAGA LIGI KUU MZUNGUKO WA 1

**Na Adam Fungamwango**

MZUNGUKO wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22, umemalizika Jumatano iliyopita, ukishuhudiwa jumla wa makocha 10, wakitimuliwa.

Mechi iliyochezwa Uwanja wa Manungu Complex, kati ya wenyeji Mtibwa Sugar dhidi ya Yanga, ndiyo iliyohitimisha mzunguko huo, kila timu ikicheza mechi 15. Kabla ya mechi hiyo, tayari klabu za Coastal Union na Dodoma Jiji zilitangaza kuwatimua makocha wake kutokana na kufanya vibaya kwenye mechi za Ligi Kuu.

Coastal Union iliachana na Melis Medo raia wa Marekani, huku Dodoma Jiji ikimwonyesha mlango wa kutokea, Mbwana Makata na kutimiza idadi ya makocha 10 kwa makocha kutimuliwa tangu ligi ilipoanza msimu huu, Septemba 27, mwaka jana.

Klabu nyingi kwa sasa zimekuwa zikiwatimua makocha wao kistaarabu kwa kile wanachodai ni wenyewe makocha kuandika barua ya kujiuzulu au kubwaga manyanga kwa maslahi ya pande zote mbili, lakini haiondoi ukweli kuwa hutimuliwa kutokana na matokeo mabovu. Kati ya makocha 10 waliotimuliwa, saba ni wa nje ya nchi na watatu ni Watanzania. Katika makala haya, tumekusanya orodha ya makocha wa timu za Ligi Kuu ambao tayari wameshaonyeshwa mlango wa kutokea, twende sasa...

**#1. ETIENNE NDAYIRAGIJE - GEITA GOLD**

Kocha huyu wa zamani wa klabu za Mbao FC, Azam FC na timu ya Taifa, Taifa Stars alichukuliwa na Geita Gold iliyopanda na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu huu, Agosti mwaka jana.

Alipewa jukumu la kuinoa timu hiyo akitarajiwa kufanya makubwa. Katika hali isiyokuwa ya kawaida alitimuliwa kazi miezi miwili baadaye, kisa timu haifanyi vizuri.

**#2. DIDIER GOMES - SIMBA**

Aliondoka kwenye klabu ya Simba Oktoba mwaka jana, baada ya kushindwa kuipeleka timu hiyo kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Didier Gomes, raia wa Ufaransa, alijiunga na Simba mwanzoni mwa mwaka huu akitokea Al Merrikh ya Sudan. 'Alitimuliwa kiaina', baada ya Simba kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa.

**#3. HARUNA HERERIMANA - MBEYA KWANZA**

Klabu ya Mbeya Kwanza ilimtimua kocha wake Haruna Hererimana kwa madai ya timu kupata matokeo mabovu kwenye mechi za Ligi Kuu, ikimchukua kocha wa zamani wa Mbeya City, Maka Mwalwisi. Aliichukua timu Agosti mwaka jana, lakini timu ilipofanya vibaya, viongozi hawakusubiri.

**#4. GEORGE LWANDAMINA - AZAM FC**

Kocha huyu mkongwe raia wa Zambia, alitimuliwa katikati ya Desemba mwaka jana baada ya shinikizo kubwa kutoka kwa mashabiki wa Azam FC.

Lwandamina, kocha wa zamani wa Yanga, alipewa kibarua hicho Desemba mwanzoni mwa mwaka jana, lakini baada ya kuona kila kukicha afadhali ya jana, uongozi wa Azam ukaamua akae pembeni.

**#5. JAMES OMOG - MTIBWA SUGAR**

Alitimuliwa katikati ya Desemba mwaka jana baada ya jahazi la Mtibwa Sugar kuonekana kuzama siku hadi siku. James Omog, raia wa Cameroon, kocha wa zamani wa Azam FC na Simba, aliletwa nchini ikionekana kama itakuwa suluhisho la kuboronga la Mtibwa Sugar msimu uliopita, lakini ikawa afadhali hata ya msimu uliopita kuliko huu.

**#6. HEMED MOROCCO - NAMUNGO**

Baada ya misimu miwili ya mafanikio, hatimaye Hemed Morocco naye ameondoka kwenye klabu ya Namungo. Ilikuwa ni Desemba mwaka jana alipoondoka baada ya timu kutofanya vema kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

**#7. PATRICK ODHIAMBO - BIASHARA UNITED**

Mkenya huyu ambaye kwa sasa anaifundisha Prisons, alikuwa kocha wa saba kutimuliwa kwenye Ligi Kuu. Yeye alitimuliwa na klabu ya Biashara United baada ya timu hiyo kuboronga, na nafasi yake kuchukuliwa na Vivier Bahati aliyekuwa kocha msaidizi wa Azam FC, ambaye alitimuliwa pamoja na George Lwandamina.

**#8. SALUM MAYANGA - PRISONS**

Alikuwa ni kocha wa Prisons. Naye alitimuliwa baada ya timu kuonekana haifanyi vema na badala yake, akaletwa Kocha Patrick Odhiambo ambaye naye alitoka kutimuliwa kwenye klabu ya Biashara United. Kwa sasa ndiyo kocha wa Mtibwa Sugar akichukua mikoba ya Omog, ingawa mpaka sasa hali ya Mtibwa na Prisons zote ni mbaya.

**#9. MBWANA MAKATA - DODOMA JIJI**

Kutokana na mlolongo wa matokeo yasiyoridhisha, hatimaye viongozi wa Dodoma Jiji, Jumatano iliyopita walitangaza kumtupia virago kocha Mbwana Makata, ambaye aliipandisha daraja timu hiyo inayocheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu.

**#10. MELIS MEDO - COASTAL UNION**

Tangu mwaka huu uanze, Coastal Union haijashinda mechi yoyote ile ya Ligi Kuu zaidi ya mechi mbili tu za Kombe la FA.

Kutinga robo fainali ya Kombe la FA, hakukuwafanya viongozi wa timu hiyo kukaa kimya, zaidi ya kutangaza kumtimua kocha Medo Jumatano iliyopita, huku ikisaka kocha mwingine.

**JE, WAJUA?**

WIKI iliyopita Manchester United iliweka rekodi ya kushinda jumla ya mechi 700 kwenye Ligi Kuu England baada ya ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Leeds United. Mechi 399 wakishinda Old Trafford na zilizosalia viwanja vya ugenini, hata hivyo dimba pekee ambalo United wamecheza michezo mingi na hawajawahi kushinda ni Uwanja wa John Smith's wa Huddersfield Town.







Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maaridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), baada ya viongozi na wanachama wa jumuiya hiyo kuchangia damu kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Maridhiano yatakayofanyika kitaifa Machi 3, mwaka huu, mkoani Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mtaka aziagiza h/shauri ulinzi miundombinu anwani za makazi

**Na Paul Mabeja,** BAHI

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewaagiza viongozi wa halmashauri zote za mkoa huo kuandaa sheria ndogo ambazo zitatumika kulinda miundombinu ya anwani za makazi zinazowekwa hivi sasa.

Mtaka, aliyasema hayo juzi wilayani Bahi alipokuwa akizindua uwekaji wa alama za mitaa, barabara pamoja na vibao vya namba za nyumba.

Alisema pamoja na wilaya zote za mkoa wa Dodoma kuanza kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan katika uwekaji wa anwani za makazi, lakini ipo haja ya kutungwa kwa sheria ambazo zitasaidia kulinda miundombinu hiyo.

"Lazima wakuu wa wilaya, wakurugenzi pamoja na baraza la madiwani kuona ni jinsi gani mnaanza kuandaa sheria ndogo ndogo zitakazolinda miundombinu hii ili yeyote atakayebainika kung'oa vyuma hivi vyenye majina na mitaa na kwenda kuviuza kama vyuma chakavu kukamatwa na kushtakiwa kwa mujibu wa sheria."

"Hivi vyuma ambavyo tunatumia kuweka majina ya mitaa ni nyara za wilaya hivyo kwa yeyote atakayebainika kuiba ni lazima tuwe na sheria ya kuwabana aliyeuza na aliyenunua," alisema Mtaka.

Aidha, alisema hali hiyo ya kutungwa kwa sheria itasaidia kuondokana na adha ambazo Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) wanakumbana nayo ya watu kuiba alama za barabarani.

"Unakuta kuna alama zimewekwa na TANROADS kuwa hapa kuna kivuko cha mifugo watu wanang'oa na kwenda kuuza vyuma chakavu sasa hivi ambavyo tunaviweka hapa leo lazima tuvitungine sheria kuvilinda,"alisema.

Vilevile, aliwataka wananchi kuwa mstari wa mbele katika kulinda miundombinu hiyo ambayo imetumia fedha nyingi.

"Mwenyekiti wa mtaa, kijiji, kitongoji lazima uwe na uchungu na miundombinu hii haiwezakani leo unaona mtu amebeba chuma hichi unamwangalia tuu, kamata weka ndani aeleze kakitoa wapi hivi ni nyara pia za kijiji lazima watu waziheshimu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema mpango huo wa uwekaji anwani za makazi wanatarajia kukamilisha ndani ya wiki mbili katika vijiji vyote 59.

"Ndugu mkuu wa mkoa, sisi Bahi tayari tulishaanza utekelezaji wa maagizo ya Rais kuhusu mpango huu wa uweaji anwani za makazi katika maeneo yote na tayari kwa kiasi kikubwa mambo yote ya muhimu tumeshayakamilisha,"alisema.

# Watakaolipwa fidia ya barabara washauriwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, amewataka wananchi waliopitiwa na barabara ya njia nne ambao watakaolipwa fedha kuwekeza kwenye kilimo cha zabibu, ufugaji na uvuvi badala ya kuzitumia kwa anasa zisizo na tija. Shekimweri alitoa ushauri huo alipokuwa akizungumza na wakazi wa Mtaa wa Vikonje na Mtumba Kata ya Mtumba Jiji la Dodoma.

Alisema pamoja na kuwekeza pia wanunue ardhi nyingine.

"Mfano, wanapewa Sh. milioni 40 hapa kama ni wazee watu wazima awe mwanaume au mwanamke lazima atageuka kuwa kijana mwenye miaka 19 na atatafuta dogodogo na kusahau kuwa fedha hizo zinatakiwa kuwekezwa kwenye miradi mbalimbali ya kimaendeleo hapa naomba niwasisitizie mkafanye matumizi sahihi," alisema.

Akihamasisha upandaji miti, aliwataka wananchi kupanda miti ya kivuli na matunda ya kuitunza mazingira huku akisisitiza ujenzi wa makazi bora.

Pia alihamasisha wakazi wa Jiji hilo kujitokeza kwa wingi kwenye sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti mwaka huu ili serikali itimize malengo yake ya kupanga maendeleo kulingana na idadi ya watu.

# Bahi yaelekezwa kuingiza mil. 50/- mfuko wa elimu

**Na Augusta Njoji,** BAHI

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Bahi mkoani Dodoma limeagiza kuingiza Sh. milioni 50 kwenye mfuko wa elimu ili kusaidia mahitaji muhimu wanafunzi wasio na uwezo ambao wamefaulu kuendelea na masomo ya sekondari.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika kikao cha mapitio ya utekelezaji wa bajeti wilayani humo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Donald Mejitii, alisema walishapitisha kwenye kikao cha baraza muda mrefu kuwekwa fedha kwenye mfuko huo lakini hadi sasa mfuko una Sh. milioni 10.

"Huu mfuko tuliuanzisha kwa dhamira njema kabisa usaidie mahitaji kwa wanafunzi wetu wanaofaulu na hawana uwezo, na ili kulifanikisha hili tuliamua kwenye baraza kuongeza ushuru wa ng'ombe kutoka Sh. 2,000 hadi 4,000 ili nyongeza hiyo iingie kwenye mfuko lakini utekelezaji wake umekuwa ukisuasua," alisema.

Awali wakizungumza kwenye kikao, Diwani wa Kata ya Ibugule, Blandina Magawa, alisema ucheleweshaji wa fedha katika mfuko huo kunasababisha wanafunzi kushindwa kuripoti shuleni kwa wakati kwa kukosa mahitaji kama sare za shule, madaftari, viatu na fedha za kujikimu kwa wanafunzi waliochaguliwa shule za bweni.

"Na tuweke tu sawa fedha hii sio hisani, ni fedha ambazo mwananchi mwenyewe anachangia kama ushuru lakini mwishoni anajua kabisa zinakuja kuwasaidia watoto walengwa, sasa tunavyosuasua kwenye utekelezaji wake hatufanyi sawa," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji, Sostenes Mpandu, alisema dhamira njema ya serikali ya kujenga madarasa, kuajiri walimu haitaweza kuleta matokeo chanya kama watashindwa kuendeleza utaratibu ambao wao wenyewe wameuweka.

"Wazazi wasio na uwezo tulishawazoesha kuwasaidia mzigo walionao ili watoto wetu waripoti shule kwa wakati, sasa kwa mwenendo huu nadhani sio sawa, matokeo yametoka wazazi wanajua mfuko wao upo lakini mpaka sasa kimya," alisema.

Akijibu hoja za madiwani, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Athumani Masasi, aliahidi hadi mwezi Machi mwaka huu kiasi hicho cha fedha kitakuwa kwenye akaunti ya mfuko na watoto wote wanufaika watapata mahitaji yao.

"Nikiri sikuwa nimepata suala hili kwa haraka kujua utaratibu wake umekaaje, niiombe kamati ya elimu ikutane Jumatatu kupitia majina ya walengwa na idadi itakayopatikana waanze kupewa mahitaji yao, na hapa niwaahidi katika makusanyo ya mapato ya ajenda ya kwanza itakuwa watoto kwenda shule," alisisitiza.

Akihitimisha hoja hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alielekeza fedha hizo kutolewa haraka ili watoto waende shule.

"Fedha hizi zimechelewa sana kutolewa, na ndio maana kwenye mahudhurio tunaona kuna watoto zaidi ya 1,000 hawapo shuleni na inawezekana sababu mojawapo ni kukosa mahitaji kwa watoto ambao



# Polisi yaomba ushirikiano wa kudhibiti uhalifu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewataka viongozi wa kata na vijiji kushirikiana na jeshi hilo kudhibiti matukio ya uvunjifu wa amani yakiwamo mauaji.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alitoa ombi hilo juzi kwenye mkutano maalumu na maofisa watendaji wa kata wa Wilaya ya Mbeya.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kuwatambulisha wakaguzi kata wa jeshi hilo waliopangwa kwenye kata zao pamoja na kutoa elimu ya kukabiliana na matukio ya uhalifu kwenye jamii ikiwamo kusuluhisha migogoro kwa haki.

Kamanda Matei alisema lengo la kuwapanga maofisa hao kwenye kata ni utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro la kuongeza nguvu ya kukabiliana na matukio ya uhalifu kwenye jamii.

Alisema kazi ya maofisa hao wa polisi kwenye kata ni pamoja na kushirikiana na vikundi vya ulinzi shirikishi (Sungusungu) kulinda na kuwadhibiti wahalifu.

"Tunaomba tushirikiane kukabiliana na matukio haya ya uhalifu kwenye maeneo yetu, mkisuluhisha migogoro kwa hali mtasaidia kupunguza matukio haya ya uhalifu kwenye maeneo yenu, ukishindwa kuusuluhisha mgogoro husika unaupeleka ngazi ya juu yako," alisema Kamanda Matei.

Alisema matukio ya uhalifu yanapoongezeka kwenye jamii yanasababisha kukwama kwa shughuli za maendeleo na kusababisha wananchi kuishi kwa hofu.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu Wilaya ya Mbeya, Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Vincent Mbua, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kuwapeleka wakaguzi kwenye Kata huku akiahidi kwamba serikali itashirikiana nao.

Aliwaagiza maofisa watendaji wa kata zote za wilaya hiyo kuhakikisha wanawatafutia wakaguzi hao ofisi za kufanyia kazi ili wafanye kazi kwa uhuru na kwa weledi.

# Tulia alivyopokelewa kifalme

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mkoa wa Mbeya juzi walimpokea kama mfalme Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson ambaye aliwasili kwa mara ya kwanza jijini humo tangu alipochaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dk. Tulia alianza kupata mapokezi kuanzia alipoingia mkoani Iringa ambapo wananchi walimsimamisha katika maeneo mbalimbali na wakiwa wamebeba mabango yenye ujumbe mbalimbali wa kumpongeza kwa kuchaguliwa.

Katika Mkoa wa Mbeya alianza kupokea mapokezi ya wananchi katika Mji wa Igawa wilayani Mbarali ambapo viongozi na wanachaka wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) walikuwa wanamsubiri kwa ajili ya kumpokea.

Msafara wake ulisimamishwa na wananchi katika maeneo tofauti ya mkoa huo mpaka ulipowasili katika Uwanja wa CCM Ruanda Nzovwe jijini Mbeya ambapo uliandaliwa mkutano maalumu wa kuzungumza na wananchi.

Akizungumza na wananchi baada ya kupokelewa katika uwanja huo, Dk. Tulia aliwashukuru wananchi kwa kumwamini wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2020 kwa maelezo kuwa kuchaguliwa kwake ndiko kulikompa sifa ya kwanza ya kuwania nafasi ya uspika.

Alisema atahakikisha anaendelea kushirikiana na wananchi pamoja na viongozi wa Mkoa wa Mbeya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya mkoa huo.

Alisema atahakikisha vipaumbele mbalimbali vya mkoa huo vinatekelezwa ukiwamo upanuzi wa Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) katikati ya Jiji la Mbeya na kuifanya iwe ya njia nne ili kuondoa msongamano.

"Ninawahakikishia ndugu zangu mkataba wa kuanza upanuzi wa barabara hii utasainiwa kabla bajeti ya mwaka 2022/2023 haijapitishwa, kwa hiyo ndugu zangu naomba tuendelee kushirikiana kama mlivyonipokea vizuri," alisema Dk. Tulia.

Alisema atahakikisha anauongoza mhimili wa Bunge kwa kufuata kanuni na taratibu za mhimili huo ili kuhakikisha taifa linapata maendeleo ambayo yanakusudiwa.

Vilevile, Dk. Tulia aliwashukuru wabunge wote kwa kumchagua kwa asilimia 100 kuwa Spika huku akiwataka waendelee kushirikiana naye kama walivyoshirikiana naye wakati akiwa Naibu Spika wa mhimili huo.

Mwenyekiti wa wabunge wa Mkoa wa Mbeya, Oran Njeza, alimwomba kiongozi huyo kuendelea kushirikiana na wabunge wenzake wa mkoa huo kuongeza msukumo wa miradi ya maendeleo.

Alisema Mkoa wa Mbeya bado una idadi ndogo ya viwanda hali ambayo inasababisha uhaba wa ajira kwa vijana na hivyo akaiomba serikali kutenga eneo kwa ajili ya viwanda.

Vilevile alimwomba Dk. Tulia kuongeza msukumo kwenye uboreshaji wa miundombinu ya barabara akidai kuwa barabara nyingi za mkoa huo haziko katika hali nzuri hali ambayo inakwamisha shughuli za maendeleo.

"Tuna eneo la Tanganyika Pakers lipo wazi kwa sasa na halizalishi chochote, sasa tunaomba utusaidie kuongeza msukumo wa kulitumia eneo lile kwa ajili ya viwanda," alisema Njeza.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, alisema kuchaguliwa kwa Dk. Tulia kuwa Spika kumesababisha mkoa huo kupata Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya chama hicho Taifa.

Alisema mkoa huo haujawahi kupata mjumbe kwenye kamati hiyo kwa kipindi cha miaka 30, hivyo wamepata heshima kubwa ya kuwa na mjumbe wa kamati hiyo.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akiwahutubia wananchi wa Jiji la Mbeya waliojitokeza kumpokea juzi kwenye Uwanja wa Ruanda Nzovwe ikiwa ni mara ya kwanza kuwasili mkoani Mbeya tangu alipochaguliwa kushika wadhifa huo, wengine ni wabunge wa majimbo mbalimbali nchini. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Rungwe yaweka mikakati kuongeza uzalishaji wa vanila

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WILAYA ya Rungwe kwa kushirikiana na wadau wa kilimo imeanza mikakati maalumu la kuhamasisha wananchi kulima vanila ili kulifanya zao hilo kuwa miongoni mwa mazao makuu ya biashara na kuongeza kipato kwa wananchi.

Ofisa Kilimo wa Wilaya hiyo, Juma Mzara, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati maofisa wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la HELVETAS walipokagua shamba darasa la zao hilo lililoko katika Kijiji cha Sogea wilayani humo.

Alisema wanaendelea kuhamasisha wananchi kulima zao hilo kutokana na wilaya hiyo kuwa na hali nzuri ya hewa ambayo inaruhusu zao hilo kustawi.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo wamekuwa wakizalisha mazao mbalimbali zikiwamo ndizi, chai, viazi mviringo, maparachichi na kakao katika baadhi ya maeneo, lakini vanilla ni zao geni kwao.

Alisema zao hilo ni miongoni mwa mazao yenye bei kubwa duniani kwa sasa, hivyo wananchi wakizalisha vizuri watapata mavuno mengi na kupata kipato cha kuinua maisha yao.

"Mwitikio wa wananchi bado ni mdogo lakini hii ni kwa sababu ni zao geni kwao, tuna imani kwamba baada ya mavuno kuanza wengi watahamasika kulima zaidi maana baadhi huwa wanataka waone kwanza mafanikio," alisema Mzara.

Mtaalamu wa kilimo cha vanilla anayesimamia Mkoa wa Mbeya, Daud Mwalulesa alisema tangu walipoanza kuhamasisha kilimo cha zao hilo imepita miaka mitatu na kwamba mpaka sasa watu wanaohitaji kulima zao hilo wamefikia 800.

Alisema wakulima hao wamekuwa wakipatiwa miche kuanzia 50 mpaka 150 na kwamba kwa wenye uwezo huwa wanpewa miche mingi zaidi ili kuongeza uzalishaji.

Alisema mpaka sasa baadhi ya wakulima walioanza muda mrefu kulima zao hilo tayari wana uwezo wa kuongeza miche bila kutegemea micha ya kupewa na serikali kwa sababu wana uwezo wa kutumia vikonyo.


"Tatizo kubwa ambalo huwa linatukabili ni ukosefu wa vyombo vya usafili kwenda kuwatembelea wakulima maana maofisa kilimo wamepewa kila mmoja eneo lake la kusimamia na wakulima unakuta wametawanyika," alisema Mwalulesa.

Alisema usimamizi wa zao hilo ni mgumu kwa sababu inatakiwa mkulima kutumia muda mwingi kuliangalia pamoja na kufanya uchavushaji kwa kutumia mikono yake tofauti na mazao mengine.

Mkurugenzi wa Shirika la HELVETAS, Daniel Kalimbiya, alisema shirika hilo ambalo ni miongoni mwa watekelezaji wa Program ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa chai na mazao ya bustani ya AGRI-CONNECT litaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Rungwe kuboresha zao hilo.

Alisema wataendelea kushirikiana na serikali kwenye zao hilo kama ambavyo inashiriki kwenye mazao mengine kama maparachichi na matunda mengine.





Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Dk. Tulia Ackson, alipofika ofisini kwake Vuga kujitambulisha ikiwa ni mara ya kwanza baada ya kuchaguliwa kushika wadhifa huo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZEC yazindua mpango mkakati uchaguzi mkuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), imezindua mpango mkakati wa uchaguzi mkuu kwa kipindi cha miaka mitano 2022/2026 ikiwashirikisha wadau mbalimbali wa uchaguzi ikiwamo wawakilishi wa vyama vya siasa.

Katika hotuba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera Uratibu na Shughuli za Baraza la Wawakilishi, iliyosomwa na Mkurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa wizara hiyo, Khamis Haji Khamis, alisema ni jambo la msingi kuwashirikisha wadau wao kwa kila hatua ya utekelezaji wa mpango ili kutowaacha nyuma.

Hayo yalisemwa katika uzinduzi huo, uliofanyika ofisi za tume hiyo, Maisara Mjini Zanzibar.

Alisema wanaweza kuwa na mkakati mzuri, lakini utekelezaji wake ukasuasua hivyo ni jambo la msingi kuhakikisha wanausimamia kikamilifu ili kutoa matunda.

Aidha, alisema pamoja na kuwa na mpango mkakati wa miaka mitano, lakini yapo mambo yanayoibuka katikati ya mipango yao hivyo ni wajibu kwa viongozi wa ZEC kuona wanazuia mambo hayo ili yasiwatoe katika makusudio yao.

Mkurugenzi wa ZEC, Khamis Kona Khamis, alisema mchakato wa kuandaa mkakati huo ulianza mwishoni mwa mwaka 2021 baada ya kumalizika kwa muda wa utekelezaji wa mpango mkakati wa mwaka 2015-2019.

Alisema ZEC baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ilifanya tathmini na kuona ipo haja ya kuwa na mpango mkakati mpya kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Alisema hatua zilizopitiwa hadi kukamilika kwa mpango mkakati huo ni kufanya mapitio ya mpango mkakati uliomaliza muda kwa kubainisha mafanikio na mapungufu.

Vilevile alisema ZEC kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa inayoshughulika na mifuo ya uchaguzi iliendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe na watendaji wake kuhusu utayarishaji wa mpango mkakati huo.

Hatua nyingine alisema ni kuainisha mambo muhimu katika kuandaa mpango mkakati huo ambayo yalijumuisha dira, dhamira, nguzo, malengo makuu, malengo mkakati na shughuli zake nyingine muhimu.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Mabrouk Jabu Makame, alisema ZEC iliwashirikisha wadau wakiwemo vyama vya siasa, tasisi za serikali na asasi za kiraia kwa ajili ya kutoa maoni yao kwa lengo la kupata mkakati uliobora wa utekelezaji wa majukumu yake.

Alisema ZEC inathamini michango na jitihada zote zinazotolewa na wadau wa uchaguzi ambao walishiriki katika uandaaji wa mpango huo.

Hivyo, aliwaomba wadau wote wa uchaguzi kuipitia kwa makini nakala ya mpango mkakati huo ili kuishauri tume namna bora ya utekelezaji wa yale yotee yaliyoainishwa katika mpango huo.

Mwakilishi kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Mifumo ya Kiuchaguzi (IFES) Paul Anderson, alisema kutayarisha mpango mkakati si kazi rahisi hivyo anaipongeza ZEC katika kuandaa mpango mkakati huo ambao utatoa mwongozo katika kipindi cha miaka mitano.

Akizungumza kwa niaba ya wadau wa uchaguzi, Ameir Hassan Ameir, kutoka Chama cha Demokrasia Makini (CDM), alipongeza hatua ya kushirikishwa katika mpango mkakati huo na imani yao kuona yale yote waliyokubaliana yatafanyiwa kazi kwa maslahi ya Zanzibar na demokrasia Tanzania.

## Makamu wa Rais ampa kongole Spika Tulia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amempongeza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson kwa jitihada anayoendelea kuionyesha katika kuliongoza Bunge kwa maslahi ya Taifa.

Hemed aliyasema hayo ofisini kwake Vuga Mjini Zanzibar, wakati alipofanya mazungumzo na Spika huyo alipofika kujitambulisha kwa mara ya kwanza tokea achaguliwe kushika nyadhifa hiyo.

Hemed alisema Serikali ya Tanzania inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan ina imani kubwa na utendaji kazi wake ndani na nje ya Bunge anaoendelea kuionyesha kwa maslahi ya Watanzania.

Aidha, alisema serikali itatoa ushirikiano wa hali ya juu ili kufanya kazi kwa ufanisi na kuwaletea maendeleo wananchi.

Hemed alisema kuwa muhimili wa Bunge ni muhimu ambao una uwakilishi wa Watanzania wote hivyo ana imani muhimili huo utasimamia kanuni na sheria zilizopo ili kulinda maslahi ya wananchi.

Kwa upende wake Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson, alisema kuwa Bunge analoliongoza lina ushirikiano wa karibu na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ili kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania.

Dk. Tulia alisema kuwa Bunge lipo tayari kupokea maelekezo yanayotolewa na viongozi wakuu wa nchi ili kufikia malengo waliojipangia ya kuwahudumia wananchi waliowachagua ambao wana matumaini makubwa kupitia chombo hicho cha kutunga na kubadilisha sheria kwa maslahi ya Watanzania kwa ujumla.

# Ataka kadi mpya za CCM kuwafikia wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Sadalla, amewataka viongozi wa chama hicho Wilaya ya Kusini Unguja kuhakikisha kadi mpya za uanachama za elektroniki zinawafikia wanachama wote wenye sifa na vigezo vya kupata kadi hizo.

Wito huo aliutoa katika hafla ya uzinduzi wa ugawaji wa kadi hizo katika wilaya ya Kusini Unguja, akisisitiza kuwa lengo la kadi hizo ni kuwafikia wanachama haraka ili zitumike katika shughuli za chama.

Alieleza kuwa CCM ni taasisi ya kisiasa inayoenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, ndio maana ikaweka mfumo imara wa kadi za kisasa zinazohifadhi kumbukumbu zote za wanachama wake.

"Matarajio yetu ni kuwa kadi hizi hazitokaa maofisini mwenu, hakikisheni kila mwanachama anayestahiki kupata kadi anapewa bila vikwazo," alisisitiza Dk. Mabodi.

Dk. Mabodi, alieleza kuwa ugawaji wa kadi hizo ni mwendelezo wa uzinduzi wa kadi uliotekelezwa hivi karibuni na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan katika kilele cha kuadhimisha miaka 45 ya kuzaliwa kwa CCM kilichofanyika mkoani Mara.

Naibu Katibu Mkuu huyo aliwasihi wanachama, viongozi, watendaji na makada wa CCM kuhakikisha wanazitunza vizuri kadi hizo kwa kuwa uzalishaji wake ni gharama kubwa.

Alisema hatua kubwa za kimaendeleo katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii zilizofikiwa na CCM, zinatakiwa kwenda sambamba kasi ya wanachama kukitumikia chama bila kuchoka.

Pamoja na hayo aliwataka wanachama waliokabidhiwa kadi kuendelea kusimamia na kuishi katika Itikadi ya CCM ya ujamaa na kujitegemea.

"Chama Cha Mapinduzi ni itikadi inayoaminika kutoka moyoni, hivyo endeleeni kujitoa kwa ari na mali kukitumikia chama chetu bila kujali vikwazo vyovyote viwe vya kimazingira au baadhi ya watu wasiopenda maendeleo yetu", alisema Dk. Mabodi.

Alisisitiza kwamba itikadi ya CCM ndiyo inayoamua masuala yote muhimu ya maendeleo ya nchi zikiwamo uimarishaji wa huduma za afya, elimu, kilimo bora, maji safi na salama, miundombinu ya barabarani, majini, angani na nchi kavu.

Aliwataka wanachama wa zamani kuwaenzi na kuwaheshimu wanachama wapya kwani ndani ya CCM hakuna ubaguzi, wanachama wote wana haki sawa.

Akizungumzia uchaguzi mkuu wa chama Dk. Mabodi, aliwakemea baadhi ya wanachama walioanza kutengeneza makundi ya kukigawa chama wa kuwafanyia kampeni za siri baadhi ya watu wakati bado viongozi wa chama na serikali hawajamaliza muda wao wa uongozi.

Dk. Mabodi aliwasisitiza wanachama na wananchi kwa ujumla kujitokeza kwa wingi kuhesabiwa katika sensa ya mwaka 2022 ili serikali iweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa takwimu sahihi ya watu na demografia.

Naibu Katibu Mkuu huyo, alikemea vitendo vya udhalilishaji na kuwataka wanachama na wananchi wa Wilaya ya kusini kupinga vitendo hivyo na kuhakikisha wanaendelea kuishi katika maadili, mila na desturi sahihi za Kizanzibari.

Kwa upande wake Katibu wa CCM Mkoa wa Kusini Unguja, Amina Imbo, alisema walipokea kadi mpya 4,000 ambapo Wilaya ya Kusini Unguja wamepewa kadi 1,782 na wilaya ya kati walipewa kadi 2,218.

Naye Katibu wa CCM Wilaya hiyo, Asha Mzee, alisema wanachama wote ni 14,484 ambapo waliosajiliwa awali ni 8,800 na usajili mpya ni 1,140 na waliosajiliwa mpaka sasa ni wanachama 9,940.

HABARI KITAIFA

# Bilioni 7.8/- kupeleka majisafi halmashauri 3

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA) imepokea Sh. bilioni 7.8 kwa ajili ya kupelekea huduma ya majisafi na salama katika Halmashauri za Msalala, Usheu na Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Allen Marwa, wakati akitoa taarifa ya usambazaji wa mtandao wa maji Kata ya Mwendakulima wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na fedha za serikali.

Alisema wamepokea Sh. bilioni 7.8 kati ya hizo Sh. milioni 518 ni fedha zinazotokana na UVIKO - 19 ambazo zitatumika kufanikisha ujenzi wa mtandao wa maji katika mtaa wa Mwime Makungu wenye urefu wa kilometa 26 hivyo kila mwananchi atanufaika na mradi wa maji wa Ziwa Viktoria.

Marwa alisema, katika mradi huo usambazaji wa maombi ya maji yameshasambazwa katika maeneo mbalimbali na baadhi ya wakazi wanaendelea kunufaika na mradi huo na mpaka hivi sasa umeshatekelezwa kwa zaidi ya asilimia 56 na unatarajia kukamilika mwezi ujao.

Alisema, fedha hizo zinatarajia kuwanufaika pia wakazi wa Kata ya Ngogwa ambapo jumla ya wakazi 16,000 walioko katika eneo hilo watanufaika na mradi kwani mpaka hivi sasa wameshajenga matangi ya kuhifadhi majisafi na salama na kufikia mwaka 2025 watakuwa wameshawafikia wananchi kwa asilimia 95.

Hata hivyo Marwa alisema, katika Halmashauri ya Ushetu serikali imetoa Sh. milioni 150,000 kwa ajili ya utafiti wa upelekaji wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria kuwataka wananchi kuwa na subira na kuwa na imaji kwa sababu huduma ya majisafi na salama utawafikiwa wakati wowote.

Naye Hamadi Mwinyi, mkazi wa Mtaa wa Mwime, alisema, awali mtaa ulikuwa hauna huduma ya majisafi na salama na malalamiko yalikuwa mengi kwa wananchi na walilazimika kutumia maji ya kwenye visima ambavyo sio salama kiafya na kwamba kama kunamiradi mengine ya maendeleo wapelekewe.

Alisema, wakati wa kiangazi kisima kimoja kilikuwa kikitumiwa na kaya zaidi ya 20 hali ambayo ilikuwa ikisababisha vilikuwa havitoshelezi mahitaji ya wananchi na kwa uwepo wa mradi huo utasaidia kuondoa changamoto waliyokuwa nayo na kutumia maji safi na salama na kuondokana na magonjwa ya mlipuko.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga alisema, wilaya ina maji ya kutosha na serikali imeshakwisha kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya kupeleka maji kwa wananchi na kufikia mwaka 2025 maji yatakuwa yamewafikia wananchi wote wa Ushetu, Kahama Manispaa na Msalala kwa asilimia 95.



Wafanyakazi wa Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), wakiorodhesha majina ya watu ambao wako tayari kupata chanjo ya kujikinga na corona, katika kituo cha daladala cha Feri jijini Dar es Salaam juzi. Mbali na kutetea abiria, chama hicho kwa sasa kinafanya kampeni ya chanjo ya ugonjwa huo katika maeneo mbalimbali nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ufaransa yampa medali m'biashara

**Na Beatrice Shayo**

UBALOZI wa Ufaransa nchini umempatia medali ya heshima mfanyabiashara maarufu nchini Jitesh Ladwa, kutokana na mchango wake kwa jamii katika shughuli zake za maendeleo kwa Ufaransa, Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Ladwa alikabidhiwa medali hiyo ijulikanayo Kama "The Legion of Honor" mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, kwa niaba ya Rais wa nchi hiyo.

Katika hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali akiwamo Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda na wafanyabiashara wenzake Ladwa. Balozi Hajlaoui alisema medali hiyo ni kubwa nchini Ufaransa na ulimwenguni imekuwa ikitolewa kwa wananchi wa nchi hiyo na wageni kutokana na machango huo mkubwa kwa maendeleo ya nchi hizo.

Aidha, miradi ya ushirikiano kupitia Lwada ni kielelezo tosha cha urafiki kati ya Tanzania na Ufaransa, na ziara ya hivi karibuni ya Rais Samia Suluhu nchini Ufaransa ilikuwa ya kihistoria na ya kifahari.

Ladwa alishukuru kwa medali aliyopata ambayo anakiri hakutarajia na kutaka Watanzania kujikita katika maendeleo. Alisema ziara ya hivi karibuni ya Rais Samia Suluhu Hassan iliyofanikiwa nchini Ufaransa ni kielelezo tosha cha ushirikiano mkubwa kati ya Tanzania na Ufaransa.

Alisema Ufaransa ina mchango mkubwa katika uwekezaji, ushirikiano wa kiusalama na maendeleo ya kiuchumi kwa juhudi na miradi mikubwa nchini Tanzania.

# TARURA yasaidia wakulima kufikisha mazao

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

WAKUU wa Kongani za Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) za Mbarali na Ihemi zinahudumia mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe na Iringa, wamepongeza huduma za Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kwa kuboresha barabara za vijijini.

Wamesema hatia hiyo imeinua ufanisi wa kilimo katika mikoa hiyo mitatu.

Katika taarifa zao walizopata waandishi wa habari za kilimo mjini hapo, wakuu hao wameipongeza serikali kwa kupasua barabara hadi mashambani na nyingi kuziimarisha kwa ngazi ya changarawe.

"Sekta ya kilimo ina changamoto nyingi, kuanzia kuandaa mashamba, kufikisha mbegu. Mbolea na viuatilifu kwa kulima, vifaa vya kilimo na hifadhi ya mazao na hatimaye kuyafikisha mazao sokoni. Yote haya yana uhusiano na barabara; sasa barabara zimefika mashambani waliko wakulima. Haya ni maendeleo makubwa," alieleza Meneja wa Kongani ya Ihemi anayehudumia mikoa ya Iringa na Njombe, Khalid Mgalamo, na kuongeza kwamba mbali ya barabara kuwafikia wakulima wadogo serikali imeboresha sera, sheria na kanuni ili ziwe rafiki kwa wakulima.

Alieleza kuwa matokeo ya ujenzi wa barababa na maboresho ya sera za uwekezaji vimechangia kuongeza idadi ya wawekezaji katika kongani ya Ihemi hadi kufikia wawekezaji 25, zikiwamo kampuni za Green Valley Agro (GVA), Silverlands na GBRI business solutions.

Mkoa wa Iringa umeongeza vikubwa aina za barabara kutoka hali ya mwaka 2012 ambapo mkoa ulikuwa na jumla ya kilometa za rami 314, changarawe: 1,456.3, ardhi: 2,682 na jumla ya barabara ikiwa ni kilometa 4,452.

Meneja wa Kongani ya Mbarali, Tulla Mloge, inayohudumia mikoa ya Mbeya na Songwe, alisema katika mikoa yote miwili imeongeza idadi ya kilometa za barabara zinazowafikia wakulima waliko mashambani.

"Changamoto kubwa ilikuwa ni barabaza za kuyafikia masoko. TARURA imeboresha barabara nyingi za mashambani na kufanya usafirishaji wa mazao kufikia masoko kuwa rahisi," alisema Mloge, na kuongeza kwamba ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi umewasaidia wakulima kupata pembejeo kwa urahisi, kusafirisha mazao yao sokoni na kuinua kidato kwa wakulima na nchi kwa ujumla.

Mloge ameeleza sasa mazao ya Kongani ya Mbarali yanayafikia masoko ya Afrika ya Kusini, India China, Ulaya na Marekani.

"Sasa tunauza kwa uhakika zaidi maparachichi, viazi, mboga na matunda," alieleza Mloge na lakini akasema bado kuna haja ya kuhakikisha mazao haya yanapata msukumo ili yapate ubora unaokidhi viwango vya soko.

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE

# Russia yawasili kuzungumza, Ukraine yasusa, ikihofia eneo la mazungumzo

**Na Christina Mwakangale**

IKIWA leo ni siku ya tano tangu Russia kuishambulia Ukraine, jumuiya ya kimataifa imeendelea kutoa wito kwa Russia kuweka silaha chini na kurudi kwenye majadiliano, zikieleza athari za uvamizi nchini Ukraine ni kwa raia hasa watoto na wanawake.

Hadi jana takribani watu 200 wameuawa tangu mzozo huo, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya kimataifa. Amri ya raia kutotoka nje imetangazwa nchini Ukraine huku wanaume walio na umri kati ya miaka 18 wakitakiwa kusalia Ukraine, kuongeza nguvu ya kuyakabili majeshi ya Russia.

Umoja wa Mataifa (UN), umesema tayari idadi ya wakimbizi kutoka Ukraine inafikia 360,000 wengi wao wakiwa wanawake, wazee na watoto wamefika mipakani ili kuingia nchi jirani Romania, Poland, Slovakia, Moldova na Hungary, kutafuta hifadhi.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, ameendelea kutumia mitandao ya kijamii ikiwamo ukurasa wake Twitter, kujirekodi kwa video na kuhamasisha umma kujilinda dhidi ya adui, akisema atasalia nchini mwake hadi mwisho, pia hatosalimu amri.

Jana, Rais wa Russia Vladimir Putin alitia nia kufanya mazungumzo na Rais Zelensky akisema yupo tayari, licha ya baadaye kukataa kushiriki mazungumzo, akidai nchi ya Belarus ambako mkutano utafanyika si salama kwake, kwamba mipaka yake inatumika kumwingiza adui.

Kiongozi wa Belarus, Alexander Lukashenko alitia wito kwa Kyiv, jana kuhudhuria mkutano nchini mwake kuzungumza na Russia.

"Russia vitendo hivi vina kila ishara ya uhalifu wa kimbari. Inaangamiza maeneo ya miundombinu ya kiraia. Inaonyesha mlengwa wa kwanza ni mimi (serikali), pili familia yangu," anasema Zelensky.

Huku wajumbe wa mkutano wakiwasili nchini Belarus kwa mazungumzo na Ukraine, Rais Zelenskiy amekataa ombi hilo, akisema mazungumzo ya Minsk yangefanyika iwapo Russia, isingeishambulia Ukraine kutoka eneo la Belarus.

"Miji mingine inaweza kutumika kama mahali pa mazungumzo. Tunataka amani, tunataka kukutana, tunataka vita iishe. Warsaw, Bratislava, Budapest, Istanbul, Baku, ni miji mbadala tumewapa Russia.

"Jiji lingine lolote litatufaa, katika nchi, ambayo makombora yake hayarushwi dhidi yetu. Hii ndiyo njia pekee ya mazungumzo yanaweza kuwa ya ukweli na yanaweza kumaliza vita," anasema Rais Zelensky jana kwenye taarifa yake iliyorushwa na kituo cha televisheni Sky News.




Watoto wakiwa eneo la ukaguzi baada ya kuokolewa na msamaria mwema kutoka nchini Ukraine, na kuvuka mpaka wa Beregsurany ili kuingia nchini Hungary, jana. **PICHA: AP**

**Russia vitendo hivi vina kila ishara ya uhalifu wa kimbari. Inaangamiza maeneo ya miundombinu ya kiraia.**



Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky.



Rais wa Russia, Vladimir Putin.

Rais Putin, ameendelea kushikilia msimamo wake akidai kwamba lengo ni kudhoofisha uwezo wa kijeshi wa Ukraine na kuondoa utawala wa kinazi, akisema jeshi lake halilengi raia.

Russia tayari imeongezewa vikwazo vya kiuchumi kutoka jumuiya hizo, ikiwamo Marekani na Uingereza, huku nchi takribani 27 za Jumuiya ya Kujihami (NATO), zikiipatia Ukraine msaada wa vifaa vya kijeshi na kibinadamu.

Ujerumani jana iliahidi kuipatia Ukraine silaha na vizuizi vya mashambulizi ya angani 1,500 kutokana na nchi hiyo kuomba msaada kwa nchi tofauti kuisaidia vifaa vya kijeshi.

Maeneo kadhaa ya mji mkuu wa Ukraine, Kyiv yalishuhudia milio ya silaha na milipuko kutokana na majibizano ya kijeshi kwa nchi hizo mbili, huku Russia jana ikishambulia ghala la mafuta gesi lililoko Vasylkiv Kusini mwa mji huo, kililipuliwa na wanajeshi wa Russia wakishikilia miji ya Kharkiv na Kakhova.

Wakazi wa eneo hilo wametakiwa kusalia ndani na kufunga madirisha ili kuepuka harufu na moshi wenye sumu unaotoka kwenye ghala hilo kuwaathiri, baada ya kulipuliwa usiku wa kuamkia jana.

**UJERUMANI**

Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz, amesema nchi yake italinda kila kipande cha ardhi cha nchi washiriki wa Nato, iwapo Russia, itathubutu kuvamia.

"Ujerumani itailinda kila kilomita mraba ya eneo la nchi washiriki wa Nato. "Tunamaanisha," amesema Kansela Scholz akizungumzia mzozo huo, kwenye hotuba yake bungeni jijini Berlin, kupitia kituo cha televisheni Aljazeera.

Amesema tayari Ujerumani imepeleka vikosi nchi jirani na Ukraine, ambazo ni sehemu ya Nato, kuimarisha ulinzi na kwamba bajeti ya mwaka huu ya nchi itatenga euro bilioni 100 kwa masuala ya ulinzi na Pato la Taifa 'GDP' kwa asilimia mbili litakwenda ulinzi.

Amesema Ujerumani itanunua mafuta na gesi kwenye soko la dunia, bila kujitegemea tena Russia, akisisitiza kwamba Rais Putin hapaswi kudharau maazimio ya washirika wa Ukraine.

Wiki iliyopita, Ujerumani ilisitisha uidhinishaji wa bomba la Nord Stream 2 kutokana na Russia kuivamia Ukraine, bomba la Nord Stream 2 liligharimu uero bilioni 10 kwenye mradi wa bomba hilo, huku ufadhili ukigawanyika kati ya makampuni ya nishati ya Russia na nchi za Magharibi.

Ujerumani ilitangaza kusitisha mchakato wa kutoa leseni ya bomba kati yake na Russia, uendeshaji kusimamishwa ni hatua kubwa kwa kuwa Russia, inaipatia Ulaya karibu asilimia 40 ya gesi yake, inayopatikana kutoka kwa usambazaji mkubwa Mashariki mwa Russia.

HABARI MICHEZO

# GINIKI AVUNJA REKODI ZA TIGO KILI HALF MARATHON

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKATI mbio maarufu za Kilimanjaro 2022 zikiadhimisha miaka 20 tangu kuasisiwa kwake, Watanzania wameonyesha jeuri ya hali ya juu kwa kushinda nafasi nyingi sana za juu katika msimu huu ambapo Mtanzania Emmanuel Giniki ameibuka Mshindi wa Mbio za Kilomita 21 maarufu kama Tigo Kili Half Marathon 2022 zilizofanyika mjini Moshi jana, Jumapili.

Giniki amevunja rekodi ya Mtanzania mwingine Joseph Panga aliyeibuka mshindi wa kwanza wa mwaka 2020; ambazo kwa miaka kadhaa zimekuwa zikitawaliwa na raia wa kigeni na hususan Wakenya ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakiibuka washindi.

Mshindi huyo namba moja wa Tigo Kili Half Marathon 2022, kwa upande wa wanaume ameshinda mbio kwa kishindo cha aina yake baada ya kuvunja rekodi ya mtangulizi wake, Panga aliyeshinda kwa kumaliza kwa kutumia muda wa saa 01:03:59 mwaka 2020, ambapo Giniki amemaliza mbio hizo mwaka huu kwa kutumia muda mfupi zaidi wa saa 01:00:35 na hivyo kuleta hamasa kubwa sana mbele ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, aliyekuwa mgeni rasmi kwenye mbio hizo.

Katika mbizo hizo za Tigo Kili Half Marathon 2022, Giniki amefuatiwa na Watanzania wenzake Gabriel Geay na Inyasi Sulley waliotumia muda wa 01:02:05 na 01:04:11 na kuibuka washindi wa pili na wa tatu, huku wakifuatiwa na Kaposhi Laizer na Shing'Ade Giniki wote kutoka Tanzania wakiibuka washindi wa nafasi ya nne na tano.

Kwa matokeo hayo, Tanzania imechukuwa nafasi za juu kuanzia ya kwanza hadi ya tano kwenye Tigo Kili Half Marathon 2022 wakimwacha kwa mbali Mkenya Bernard Masau aliyeshika nafasi ya sita kwa kumaliza mbio hizo kwa kutumia muda wa 01:04:56. Watanzania wameibuka washindi wa nafasi zote nane kati ya 10-bora kwa upande wa Tigo Kili Half Marathon 2022 na kuwaacha kwa mbali Wakenya walioibuka washindi wa nafasi ya sita na ya saba.

Akizungumza baada ya kumaliza mbio hizo na kuibuka mshindi wa kishindo, Giniki alisema kuwa anayo furaha kushinda mbio hizo na kuiletea heshima nchi yake jambo ambalo amekuwa akilitamani, huku akiwashukuru waandaaji na wafadhii wa mbio hizo za kiliometa 21 kwa miaka saba mfululizo sasa, Kampuni ya Tigo.

Giniki anaitaja siri ya ushindi wake ni mazoezi na kujituma, na kuendelea kufafanua anayo furaha kushinda mbio hizo na kuiletea heshima nchi yake jambo ambalo amekuwa akilitamani.

"Pamoja na kwamba mbio hizi zimekuwa zikifanyika hapa nyumbani, tumekuwa tukishindwa kuzitendea haki kwa kuwa wageni ndiyo wamekuwa wakizitawala. Ninayofuraha leo nimeweza kulitoa taifa langu kimasomaso," alisema Giniki.

Katika mbio hizo za Kili Half Marathon mwaka huu, Watanzania wameng'ara sana ikilinganishwa na miaka ya nyuma, ambapo kwa wanawake, Mkenya Agness Ngolo ameibuka mshindi wa kwanza kwa kumaliza kutumia muda wa saa 01:12:17 kwa kumpita kwa mbali kidogo Mtanzania aliyeibuka mshindi wa pili, Jackline Sakilu aliyetumia muda wa saa 01:14:50.

Akizungumza wakati wa halfa ya kukabidhi zawadi kwa washindi, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo Innocent Rwetabura, alisema kampuni yake inayofuraha kuchangia maendeleo ya michezo nchini hususan riadha ambayo pia huboresha afya.

Rwetabura alisema, Kampuni ya Tigo imekuwa mdhamini wa mbio za Kili Half Marathon kwa kipindi cha miaka saba mfululizo na kuongeza kuwa itaendelea kudhamini pamoja na kuboresha mbio hizo kila mwaka.

"Napenda kuchukua fursa hii pia kuwapongeza wabunifu na waandaaji wa mbio za Kilimanjaro Marathon kwa kutimiza miaka 20. Ni ukweli usiopingika kuwa mbio hizi toka kuanzishwa kwake zimetangaza vema fursa za utalii Tanzania hasa katika kanda hii ya Kaskazini. Pia, mbio hizi zimekuwa na mchango mkubwa kwenye sekta ya michezo, hususan riadha," analifafanua Rwetabura.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (mwenye tracksuit ya njano), Kaimu Mkurugenzi wa Tigo Tanzania, Innocent Rwetabura (kushoto) na Mkurugenzi wa Tigo Tanzania Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo (kulia), wakishiriki ufunguzi wa mbio za mwaka huu za Tigo Kili Half Marathon zilizofanyika Moshi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## UMZ yaanza vema Ligi Wanawake Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya UMZ imefungua vema pazia la Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar kwa ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya wenyeji Bungi Sisters.

Mchezo huo wa ufunguzi uliochezwa Katika Uwanja wa Bungi Mkoa wa Kusini Unguja, ukihudhuriwa pia na timu ya Taifa ya Tanzania ya Wanawake chini ya umri wa miaka 17.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Yusuph Sape, alisema ushindi huo mnono umetokana na maandalizi ya muda mrefu ikiwamo na harakati za kuitengeneza timu hiyo.

Alisema ushindi huo unampa imani timu hiyo kufanya vizuri katika miaka ijayo na kwamba ndiyo kwanza ina miaka miwili tangu kuanzishwa kwake.

"Tumecheza vizuri, wachezaji walifanya kazi nzuri Katika kipindi cha kwanza, tatizo la kukata pumzi kwa sasa linazidi kupungua kadri timu inavyocheza, hii inanipa matumaini kuwa baada ya miaka miwili itakuwa timu kali na nzuri ikilinganishwa na sasa," alisema.

Naye kocha wa timu ya Bungi Sister, Suleiman Khamis alisema kufungwa katika mchezo huo kumetokana na maandalizi finyu kuelekea michuano hiyo ya Ligi Kuu.

Alisema timu ilikuwa na muda mchache wa kufanya mazoezi jambo lililosababisha hata timu kushindwa kupata muunganiko mzuri.

Hata hivyo, alisema kwa sasa anajipanga kuelekea mchezo ujao kwa kurekebisha makosa ambayo ameyaona katika mchezo huo wa kwanza.

Ligi hiyo itaendelea leo kwa timu ya Green Queens kushuka dimbani dhidi ya Yellow Queens, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Polisi Ziwani.

## *Djuma abaini kinachoitesa Dodoma Jiji Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Dodoma Jiji, Mrundi Masoud Djuma, amesema baada ya kujiunga na timu hiyo, amebaini tatizo la kwanza ni wachezaji morali yao imeshuka, kitu ambacho kimesababisha kutofanya vema kwenye mechi zao za Ligi Kuu mfululizo.

Akizungumza baada ya kuitwaa timu hiyo iliyokuwa mikononi mwa Mbwana Makata, aliyeonyeshwa mlango wa kutokea wiki iliyopita, Djuma, ambaye alishawahi kuwa kocha msaidizi wa Klabu ya Simba, na kuna wakati akawa Kaimu Kocha Mkuu, alisema kazi yake ya kwanza ni kupambana na hali hiyo, ili wachezaji wake warudishe morali.

"Kazi ya kwanza hapa ni kupambana kurejesha morali, nilichogundua ni kwamba wachezaji wana uwezo sana, ila morali yao ilikuwa chini, sijui kwa nini, lakini unajua kama timu haipati matokeo mechi mbili au tatu mfululizo ni lazima iwe hivyo," alisema kocha huyo.

Alisema mbali na tatizo hilo, lakini atafanya marekebisho ya kasoro mbalimbali atakazoziona ili timu iwe sawa, lakini akaonya kuwa mabadiliko hayo yatakuja au kuonekana kwa mara moja.

"Haya yote ni lazima tupate muda, mabadiliko hayatokuja mara moja," alisema Djuma.

Timu ya Dodoma Jiji ambayo huu ni msimu wake wa pili kucheza Ligi Kuu, ilikuwa tishio msimu uliopita ambao ulikuwa msimu wake wa kwanza baada ya kupanda, lakini msimu huu imeonekana kuwa na mwendo wa kusuasua kiasi cha kuamua kumwondoa kocha wake Makata, ambaye ndiye aliyeipandisha Ligi Kuu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MADRID KUMSAJILI MBAPPE**

REAL Madrid inaamini inaweza kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe, 23, na nyota wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland, 21. ***(Marca)***

**BIESLA KUFUKUZWA LEEDS**

KOCHA wa Leeds United, Marcelo Bielsa yupo kwenye hatari ya kufukuzwa na klabu hiyo, huku kocha wa zamani wa RB Leipzig, Jesse Marsch akiwa na nafasi ya kuchukua mikoba yake. ***(Mail)***

**NUNEZ KUTUA LIVERPOOL**

LIVERPOOL inawania kumsajili mshambuliaji wa Benfica, Darwin Nunez, 22, raia wa Uruguay akitaka kujiunga na 'Wekundu' hao. ***(Football Insider)***

**MOYES KUMSAJILI DIAZ**

KOCHA wa West Ham, David Moyes amesema amezungumza na mshambuliaji wa Colombia, Luis Diaz, 25, wakati 'Wagonga Nyundo' hao wakitaka kumsajili mchezaji huyo. ***(Football London)***

**CONTE AMTAKA BOTMAN**

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kuwazidi Newcastle kumsajili Sven Botman kwa ushawishi wa kocha, Antonio Conte. ***(Star)***

**CHRISTENSEN KUTUA BARCA**

BARCELONA ipo mbele ya Bayern Munich kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Chelsea, Andreas Christensen, 25. ***(Mundo Deportivo)***

**ISAK AITAKA BARCELONA**

STRAIKA wa Real Sociedad na Sweden, Alexander Isak, 22, anataka kujiunga na Barcelona kuliko kwenda Arsenal. ***(Sport via Metro)***

**GAKPO ATAJWA UNITED**

KLABU ya Manchester United inamfuatilia straika wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Cody Gakpo, 22, na kiungo wa Sporting Lisbon na Ureno, Joao Palhinha, 26. ***(Mirror)***

**BAILLY KUTUA BARCA**

BARCELONA inampango wa kumsajili mlinzi wa kati, Manchester United, Eric Bailly, 22. ***(Star)***

**ARSENAL YAPEWA USHAURI**

KIUNGO wa zamani wa Arsenal, Paul Merson ameiambia klabu hiyo kumuuza winga, Bukayo Saka, 20, na kiungo, Emile Smith Rowe, 21. ***(Star via Mirror)***

**FLETCHER KWENDA MAREKANI**

STRAIKA wa England, Ashley Fletcher, 26, ambaye alijiunga na Watford kipindi cha majira ya joto kilichopita sasa anataka kujiunga na New York Red Bulls ya Ligi Kuu ya Marekani kwa mkopo. ***(Watford Observer)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ABRAMOVICH AIACHIA TIMU BODI YA CHELSEA

**Vikwazo vya vita vyamfanya akabidhi klabu kwa bodi ya wadhamini huku...**

**LONDON,** England

MMILIKI wa Klabu ya Chelsea, Mrusi Roman Abramovich amesema "nawapa bodi ya wadhamini wa Chelsea usimamizi na utunzaji" wa klabu hiyo.

**Abramovich, ambaye atasalia kuwa mmiliki wa klabu hiyo, amechukua hatua hiyo huku Urusi ikivamia Ukraine.**

Uamuzi huo ameufanya siku moja kabla ya Chelsea kucheza na Liverpool katika fainali ya Kombe la Carabao pale Wembley, jana Jumapili.

"Siku zote nimekuwa nikichukua maamuzi kwa nia njema ya klabu," alisema Abramovich katika taarifa yake.

"Nitabakia kujitolea kwa maadili haya. Ndiyo maana leo ninawapa wadhamini wa bodi ya wadhamini Chelsea usimamizi na utunzaji wa Chelsea FC.

"Ninaamini kwamba kwa sasa wako katika nafasi nzuri ya kuangalia maslahi ya klabu, wachezaji, wafanyakazi na mashabiki."

Bado haijajulikana kama Abramovich atawekewa vikwazo kama sehemu ya hatua za Serikali ya Uingereza dhidi ya Urusi.

BBC Sport inaelewa kuwa Chelsea haiuzwi, na mkopo wa pauni bilioni 1.5 ambao mmiliki wao alitoa kwa klabu haujalipwa. Abramovich ni mmoja wa watu tajiri zaidi nchini Urusi na anaaminika kuwa karibu na Rais wa Urusi, Vladimir Putin.

Aliongeza: "Wakati wa umiliki wangu wa karibu miaka 20 wa Chelsea FC, siku zote nimekuwa nikitazama jukumu langu kama mlezi wa klabu, ambayo kazi yake ni kuhakikisha kwamba tunafanikiwa kama tuwezavyo leo, na pia kujenga kwa ajili ya klabu kwa siku za usoni, huku pia ikichukua nafasi nzuri katika jamii zetu."

Bodi ya wadhamini wa Chelsea itaendesha jumuiya na idara za elimu za klabu pamoja na shughuli nyingine zote.

Wakati Abramovich akiwa Chelsea, klabu hiyo imeshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili, Ligi Kuu na Kombe la FA mara tano, Ligi ya Europa mara mbili na Kombe la Ligi mara tatu.

Mnamo Agosti 2021, walishinda Kombe la Uefa Super Cup na hivi majuzi walishinda Kombe lao la Kwanza la Klabu Bingwa Dunia, kumaanisha kwamba 'The Blues' hao wameshinda kila taji chini ya umiliki wa Abramovich.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
WEST BROMWICH
VERSUS
SWANSEA
1 | 1.71
X | 3.59
2 | 4.62

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# RAIOLA, BARCA WAJADILI USAJILI WA HAALAND

**DORTMUND,** Ujerumani

KLABU ya Barcelona imefanya kikao cha siri na wakala, Mino Raiola ambapo walizungumzia juu ya uhamisho wa wachezaji akiwamo mchezaji wa klabu ya Borussia Dortmund, Erling Haaland.

Haaland amekuwa kwenye vichwa vya habari kwa muda mrefu huku akihusishwa na klabu kadhaa kubwa za Ulaya

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway amekuwa akihusishwa na klabu nyingi kubwa Ulaya zikiwamo Barcelona, Manchester City na Real Madrid huku kwenye mkataba wake kukiwa na kipengele cha kuuzwa kwa pauni milioni 64.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na gazeti la De Telegraaf, Rais wa Klabu ya Barcelona, Joan Laporta na Mkurugenzi wa Ufundi, Jordi Cruff walikuwa na mazungumzo ya siri na Raiola kwenye ofisi yake jijini Monaco.

Pia kwenye mazungumzo hayo Barcelona waligusia uwezekano wa kumpata beki wa Klabu ya Ajax, Noussair Mazraoui.

Haaland hadi sasa amefanikiwa kufunga mabao 16 kwenye michezo 14 ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.



# Simeone asifia beki wa

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amimsifia sana Renan Lodi baada ya mlinzi huyo wa kushoto kufunga mabao mawili kwa Atletico Madrid wakati ikishinda 2-0 dhidi ya Celta Vigo.

Raia huyo wa Brazil alifunga kila kipindi, huku pasi za mwisho za mabao hayo zote zikitolewa na Geoffrey Kondogbia wakati Atletico wakijivuta hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kabla ya Barcelona kucheza dhidi ya Athletic Bilbao jana Jumapili.

Lodi alifunga mabao hayo mawili kwa mara ya kwanza kwa Atletico Madrid katika mechi 105 za mashindano yote, akiwa mlinzi pekee kufunga mabao mawili kwa mchezo mmoja tangu Simeone awe kocha wa timu hiyo.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Simeone alisifia ubora wa Lodi na kwamba mlinzi huyo ana stahi... kwenye kiwang... kwa sasa.

"Nina furaha sa... Renan," alisema... huyo wa Atletico...


"Msimu uliop... kuwa na dakika... kuliko mwaka w... kwanza, lakini... zote tulim... anaweza kuwa ... wakati mzuri ... usoni.

"Kitu cha muh... di ni kuona nam... anajituma kwa t... anavyojua kujitu...

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA



# KASEJA, KOCHA WATOA SIRI YA USHINDI POLISI TANZANIA

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**



MLINDA mlango wa Klabu ya KMC, yenye makao makuu makuu yake Kinondoni, Dar es Salaam, Juma Kaseja, amezungumzia siri ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Polisi Tanzania juzi kuwa kujipanga na mshikamano mkubwa kikosini na kwamba wataendeleza kasi hiyo kwa michezo ijayo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaseja alisema siri kubwa ya ushindi ni kutokana na mshikamano waliokuwa nao wachezaji kwa wachezaji pamoja na kufuata vema maelekezo ya kocha.

“Wachezaji walijipanga vizuri, hivyo tukafanikiwa kupata pointi zote tatu katika mchezo huo, kwetu ni furaha kuifunga Polisi Tanzania,” alisema Kaseja.

Kipa huyo aliwataka wachezaji wanzake waendelee kujiamini ili wazidi kuonyesha vipaji vyao na kuisaidia KMC kufika mbali zaidi.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa KMC, Ahmady Ally, amesema ushindi wa mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex ulioko Chamazi, Dar es Salaam wameupata kutokana na kufanyia kazi ubora na udhaifu wa Polisi Tanzania.

Ahmady alisema walifanikiwa kusoma mipango ya Polisi Tanzania kwa kuwazuia washambuliaji na kupata mbinu za kuwapita mabeki wa wapinzani wao jambo lililowapa ushindi huo mkubwa.

Alisema kwa ushindi huo wamefanikiwa kulipa kisasi cha kufungwa na timu hiyo mabao 2-0 katika mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo.

“Tuwapongeze wachezaji wetu kwa kufanyia kazi kile tulichowapa mazoezini, wamefanya kazi nzuri tumeweza kuwazuia washambuliaji wao kushindwa kutumia nafasi walizopata pamoja na kutumia makosa ya mabeki wao kupata ushindi huu,” alisema Ahmady.

Naye Kocha Msaidizi wa Polisi Tanzania, George Mketo, alisema anawapongeza KMC FC kwa kupata ushindi mkubwa wa mabao 3-0 dhidi yao.



# *Mayanga afunguka Mbeya Kwanza FC*

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Mtibwa Sugar, limesema liliwasoma wapinzani wao, Mbeya Kwanza kwa muda mrefu kabla ya kukutana nao juzi na kuibuka na ushindi wa mabao 2-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa klabu hiyo, Salum Mayanga, alisema mchezo ulikuwa mgumu, lakini walifanikiwa kuibuka na ushindi huo.

"Mchezo ulikuwa mgumu isipokuwa wachezaji wangu walitumia mbinu ambazo nimewapa wakafanikiwa kupata pointi tatu," alisema Mayanga.

Alisema wamelipa kisasi kwa timu ya Mbeya Kwanza, kutokana na mchezo wa mzunguko wa kwanza kufungwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Mabatini.

Pamoja na ushindi huo, Mtibwa Sugar bado ipo katika nafasi ya tatu kutoka mkiani ikiwa na pointi 15, mbili mbele ya Mbeya Kwanza na nne zaidi ya Tanzania Prisons inayoburuza mkia kwenye ligi hiyo inayojuisha timu 16 msimu huu.

Ikumbukwe timu mbili zitakazoburuza mkia zitashuka daraja moja kwa moja huku zitakazoshika nafasi ya 13 na 14 kwenye msimamo wa ligi hiyo, zikicheza mechi za mtoano 'play off' dhidi ya timu mbili kutoka Kundi A na B kwenye Championship kuwania nafasi mbili za kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

“1” - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
“X” - NI TIMU KUTOKA SARE
“2” - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 28/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5522 | SC Farense U23 vs FC Famalicao U23 | 3.27 | 3.56 | 1.95 |
| 14:30 | 2788 | Gol Gohar vs Sanat Naft Abadan | 1.82 | 3.15 | 5.20 |
| 14:30 | 3163 | Fajr Sepasi vs Peykan FC | 3.55 | 2.65 | 2.50 |
| 14:30 | 5491 | Havadar vs Foolad Khuzestan | 3.35 | 2.52 | 2.47 |
| 15:40 | 4180 | AL Jeel vs Jeddah Club | 2.65 | 2.89 | 2.65 |
| 16:00 | 3329 | Sabayil vs Zira | 4.05 | 3.14 | 1.87 |
| 16:00 | 4169 | Eastern Company SC vs Ceramica Cleopatra | 4.84 | 3.21 | 1.80 |
| 16:00 | 4189 | Arba Minch Kenema vs Sebeta City FC | 2.35 | 2.74 | 3.23 |
| 16:00 | 4768 | Ipswich U23 vs Swansea U23 | 1.65 | 3.96 | 4.15 |
| 16:00 | 4812 | Wigan U23 vs Sheffield Wednesday U23 | 2.39 | 3.55 | 2.50 |
| 16:30 | 5032 | Persepam MU vs Persebaya Surabaya | 3.32 | 2.84 | 2.24 |
| 16:30 | 5647 | Cagliari Youth vs Spal Youth | 1.63 | 4.06 | 4.15 |
| 17:00 | 5908 | East Bengal vs Northeast United FC | 2.27 | 3.37 | 2.75 |
| 18:15 | 5113 | AL Sahel SC vs AL Adalh | 2.46 | 2.79 | 2.99 |
| 18:30 | 1866 | Pirin Blagoevgrad vs Arda Kurdzhali | 2.20 | 3.18 | 3.03 |
| 18:30 | 4298 | Persepolis FC vs MES Rafsanjan | 1.46 | 3.61 | 7.13 |
| 18:30 | 5069 | El Ittihad Alexandria vs Talaea El Gaish | 2.62 | 2.72 | 3.07 |
| 19:00 | 3282 | Bahir Dar Kenema FC vs Ethiopia Bunna SC | 2.90 | 2.90 | 2.70 |
| 19:00 | 5594 | Zenit St Petersburg vs Rubin Kazan | 1.27 | 5.52 | 8.87 |
| 20:00 | 1016 | Cracovia vs Nieciecza KS | 1.71 | 3.47 | 4.43 |
| 20:00 | 1342 | Hapoel Kfar Saba vs Sectzya Nes Ziona | 2.46 | 2.73 | 3.37 |
| 20:00 | 1843 | Kasimpasa vs Fenerbahce | 2.61 | 3.30 | 2.56 |
| 20:00 | 2309 | Menemen Bld vs Altinordu | 2.49 | 3.36 | 2.49 |
| 20:00 | 2577 | Skra Czestochowa vs Miedz Legnica | 5.01 | 3.42 | 1.65 |
| 20:00 | 3410 | Hapoel Afula vs SC Kfar Qasem | 3.71 | 2.92 | 2.19 |
| 20:00 | 4246 | AS Ashdod vs Hapoel Raanana | 2.31 | 2.87 | 3.46 |
| 20:30 | 3403 | Apollon Smyrnis vs Atromitos | 2.81 | 2.91 | 2.66 |
| 20:30 | 5324 | PAS Giannina vs Lamia | 1.81 | 3.21 | 4.74 |
| 21:00 | 1936 | Brondby vs Sonderjyske | 1.48 | 4.34 | 5.92 |
| 21:00 | 2223 | Varzim vs CD Feirense | 2.84 | 3.19 | 2.38 |
| 21:00 | 3094 | Turkgucu Ataspor Munchen vs Saarbrucken | 4.03 | 3.59 | 1.81 |
| 21:00 | 5344 | Universitatea Cluj vs Concordia Chiajna | 2.32 | 3.04 | 2.94 |
| 21:15 | 3395 | Nazareth Ilit vs Maccabi Tel Aviv | 6.53 | 4.03 | 1.43 |
| 21:30 | 3359 | FC Winterthur vs Yverdon-Sport FC | 1.88 | 3.57 | 3.47 |
| 22:00 | 1374 | Kecskemeti TE vs Vasas SC | 2.85 | 3.29 | 2.24 |
| 22:15 | 2623 | FC Vaduz vs FC Aarau | 2.38 | 3.47 | 2.55 |
| 22:30 | 3296 | Academica vs Viseu | 2.38 | 3.22 | 2.83 |
| 22:45 | 1686 | Grenoble Foot vs Toulouse | 4.22 | 3.39 | 1.83 |
| 22:45 | 1809 | Derry City vs Sligo Rovers | 2.08 | 3.13 | 3.33 |
| 22:45 | 2013 | Annecy FC vs Orleans | 1.95 | 3.28 | 3.76 |
| 22:45 | 4399 | UCD Dublin vs Shelbourne | 4.16 | 3.33 | 1.79 |
| 22:45 | 4664 | Bohemians FC vs St Patricks | 2.45 | 3.07 | 2.73 |
| 22:45 | 5765 | Dundalk FC vs Finn Harps | 1.75 | 3.47 | 4.14 |
| 22:50 | 4461 | Atalanta vs Sampdoria | 1.45 | 4.69 | 6.39 |
| 23:00 | 2977 | Malaga vs FC Cartagena | 2.55 | 3.04 | 2.79 |
| 23:00 | 3571 | Modena vs Pescara Calcio | 1.82 | 3.40 | 4.44 |
| 23:00 | 4247 | Shamrock Rovers vs Drogheda Utd | 1.31 | 4.52 | 8.84 |
| 23:00 | 5381 | West Bromwich vs Swansea | 1.71 | 3.59 | 4.62 |
| 23:00 | 5923 | Granada vs Cadiz CF | 1.99 | 3.31 | 3.91 |
| 23:15 | 4385 | Sporting Braga vs Santa Clara | 1.52 | 4.14 | 5.72 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

ke

...li kuwa
...o hicho

...ana kwa
...a kocha
...

...pita ali-
... chache
...wake wa
... mara
...wambia
...kwenye
...siku za

...imu zai-
...na gani
...imu, na
...ma.”

# Michezo

Jumatatu Februari 28, 2022

Nipashe




Abramovich aiachia timu bodi ya Chelsea UKURASA 21

MMETISHA...



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimkabidhi hundi mshindi wa mbio za Kilimanjaro Marathon kilomita 42, Mtanzania Aloyce Simbu, baada ya kuibuka kidedea kwenye mbio hizo jana mjini Moshi. Kulia ni mshindi wa pili Mkenya, Arnold Kiptaoi (kulia) na kushoto ni mshindi wa tatu, James Tallam, ambaye ni raia wa Kenya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Nabi azidi kuonya ubingwa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema sasa ni muda wa 'vita' mpya wa kusaka pointi katika kila mechi ya Ligi Kuu huku akiwaonya wachezaji wake kutobweteke na nafasi walioko kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kabla ya mechi ya jana dhidi ya Kagera Sugar iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ilikuwa kileleni ikiwa na pointi 39, nane zaidi kwa wapinzani wao wa karibu, Simba walioko nafasi ya pili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema suala la ubingwa amekuwa akiendelea kusisitiza kwa wachezaji wake kuangalia mechi zinazowakabili kwa kuwa makini kutafuta pointi kila mchezo ambao utakuwa mbele yao.

"Mara kwa mara nimekuwa nikizungumza na watu wangu wa benchi la ufundi na wachezaji wangu kuhakikisha tunachukulia mechi zetu ni fainali kwa sababu hili duru la pili kila timu inajipanga kutafuta pointi," alisema Nabi.

Kuhusu winga Chiko Ushindi kutoonekana uwanjani, Nabi alisema, majeraha ya nyama za paja ndiyo sababu ya kumkosa katika kikosi licha ya kwamba amekuwa akimhitaji.

"Chiko ni usajili niliopendekeza na nafahamu uwezo wake, amekuwa na majeraha lazima apone kwa asilimia kubwa ili kuja kucheza katika mechi za ushindani," alisema Nabi.

# SIMBU, GINIKI WAFUNIKA WAKENYA KILI MARATHON

## Waziri Mkuu atoa neno zito, wakabidhiwa mamilioni, viwanja huku...

**Na Somoe Ng'itu,** MOSHI

MTANZANIA Aloyce Simbu ameibuka mshindi katika mbio za Kilomita 42 kwa upande wa wanaume kwa kutumia saa 2:16:31 katika mbio za Kilimanjaro Marathon 2022 zilizofanyika mjini Moshi mkoani Kilimanjaro jana.

Kwa ushindi huo, Aloyce ambaye ni mdogo wa mwanariadha mwingine maarufu nchini, Felix Simbu amepata zawadi ya Sh. milioni 4.1 pamoja na bonasi ya Sh. milioni 1.5 na zawadi ya kiwanja kilichoko Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Nafasi ya pili katika mbio hizo imechukuliwa na Arnold Kiptaoi ambaye ni Mkenya aliyetumia saa 2:17:05 huku nafasi ya tatu ikienda kwa Mkenya mwingine, James Tallam aliyetumia saa 2:17:43 huku Abraham Kipkosge pia kutoka Kenya akimaliza katika nafasi ya nne na Cosmas Kigen akimaliza nafasi ya tano, pia kutoka Kenya.

Washindi wengine kwa upande wa wanaume kuanzia nafasi ya sita ni pamoja na Kenneth Omulo kutoka Kenya, Marco Joseph, Khamis Athumani, Paul Festo wote kutoka Tanzania na Amos Kipchirchir wa Kenya.

Shelmith Muriuki kutoka Kenya aliibuka mshindi kwa upande wa wanawake katika umbali huo kwa kutumia saa 2:41:06 huku nafasi ya pili ikienda kwa Mkenya Flavious Kwamboka, Angle John wa Tanzania alishika nafasi ya tatu huku Annika Berlin raia wa Ujerumani akimaliza wanne na tano bora ilikamilishwa na Angella Mburu kutoka Kenya.

Nafasi ya sita ilikwenda kwa Banuela Katesigwa wa Tanzania, Justina Kilumelume wa Zambia, Rose Mallya (Tanzania), Laurie Eastup kutoka Marekani na namba 10 ilishikwa na Lusia Assenga wa Tanzania.

Emmanuel Giniki aliibuka mshindi katika mbio za kilomita 21 zilizodhaminiwa na Kampuni ya Tigo na kufuatiwa na Gabriel Geay huku Inyasi Sulley akimaliza katika nafasi ya tatu wakati Kaposhi Laizer alimaliza wanne.

**MAJALIWA ATOA NENO**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alianza kwa kuwashukuru wadhamini wote walioshiriki katika kufanikisha mbio hizo, watendaji pamoja na washiriki wote.

"Jambo hili ni la kujivunia sana, limekusanya watu wengi, hatuwezi kuliacha bila kujipongeza, kwa serikali ni la kuchochea michezo," alisema Majaliwa.

Alisema haya ni mashindano makubwa nchini na sasa yanapaswa kuitwa International Kilimanjaro Marathon kutokana kuhusisha washiriki kutoka mataifa mbalimbali huku yakiwa kwenye ubora wa juu.

Alisema serikali itaendelea kuwaunga mkono katika mbio hizo huku akiwapongeza washindi wote na kuwaambia mafanikio yao yametokana na jitihada walizozifanya.

"Pokeeni salamu za Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan), Makamu wa Rais Mpango pia amenitumia, hili ni jambo kubwa mno, Watanzania tumeanza kutambua umuhimu wa michezo, inatusaidia kujenga afya, pia inatufundisha namna bora ya kula," alisema Majaliwa.

Alisema kwa kuzingatia ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), serikali itajikita katika michezo hasa riadha ambayo imeiletea taifa sifa huku rekodi zake za kimataifa zilizowekwa na wanariadha wake wa zamani, Filbert Bayi na Juma Ikangaa zikiwa bado hazijavunjwa.

Aidha, alitoa angalizo la wale wanaotaka kuweka "kiberenge" cha kusaidia kupanda mlima waache na badala yake wapandaji wapande kwa njia ya asili.

Naibu Waziri wa Wizara ya Utalii na Maliasili, Mary Masanja, aliwapongeza wadhamini na washiriki wote wa mbio hizo kwa kuzifanya kuwa bora na za kuvutia.

Masanja aliwataka waandaaji kuandaa utaratibu wa washiriki wa mbio hizo kutembelea Mlima Kilimanjaro na vivutio vingine vilivyokuwa katika mkoa huu wa Kilimanjaro.

Bia ya Kilimanjaro ndio wadhamini wakuu wa mbio hizo na mwaka huu imeadhimisha miaka 20 huku wadhamini wa meza za maji wakiwa ni Absa Tanzania, Unilever Tanzania, TPC Sugar, Simba Cement, maji ya Kilimanjaro, GardaWorld Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel, Surveyed Plots Company Ltd, Bodi ya Utalii Tanzania na CMC Automobiles.

9 770856 541002 >